

UKURASA 20

**Barnaba amjibu kiadabu baba yake**

## Jafo akerwa viongozi kubeza 'Force Account'

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za...



UKURASA 5

**MAISHA** Baba, Mama na Mwana *Jumapili*

Desemba 20, 2020 Nipashe



HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15 **MAISHA NI NYUMBA**

Jinsi ya kung'arisha dirisha

**Vitumbua vya Nazi**

Ukurasa 14



**Unadhifu wa mwanamke akiwa ofisini**



Ukurasa 14


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 20, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580435


# Ruksa sasa wanandoa kumiliki hati ya ardhi

**WAZIRI** aweka bayana faida zake, Jaji Mkuu awashukia wasimamizi mirathi... *Endelea uk. 2*



Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akiwasili katika Kijiji cha Kirari wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, kuhitimisha mgogoro uliodumu kwa miaka 40 baina ya wananchi wa kijiji hicho na watawa wa Shirika la Kanisa Katoliki jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

## Mitambo ya Symbion kunadiwa kulipa bil. 12 madai wafanyakazi

UKURASA 2

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**MAJALIWA ACHUKIZWA BANDARI KUTOFANYA KAZI MIAKA MITATU**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameipa wiki mbili kuanzia juzi Mamlaka ya Bandari (TPA) ihakikishe...

**UKURASA WA 4**

**WAUGUZI WACHUNGUZWA TUHUMA KUUZA DAWA NA KUPOKEA RUSHWA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Katavi, inachunguza tuhuma za wizi wa dawa, kuomba...

**Wakuu mikoa, wilaya wahaha ujenzi vyumba vya madarasa**

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA VS MAJIMAJI, YANGA NA SINGIDA FA UK. 24

MAONI, KATUNI UK.6

## Jaji Mkuu awaonya wasimamizi mirathi

**Na Sabato Kasika**

JAJI Mkuu wa Tanzania, amesema wasimamizi wa mirathi ni chanzo cha kuwapo kwa mashauri mengi ya madai katika mahakama mbalimbali nchini kutokana na kushindwa kugawa vizuri mali za marehemu na kufunga mirathi.

Vilevile, amesema eneo la mirathi limegubikwa na uadui au kutoelewana kwa ndugu na jamaa kunakochangia kutokubaliana na uamuzi wa mahakama za mwanzo ama zinazosikiliza mirathi. Amesema hali hiyo inawafanya wahusika kushindana kwa kufungua mashauri ya rufani au maombi mbalimbali katika mahakama za juu. Profesa Ibrahim Juma aliyasema hayo juzi alipofungua kikao cha kamati ya kitaifa ya kusukuma mashauri ya madai kilichokutanisha wadau mbalimbali.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, alisema tatizo kubwa katika mirathi huwa linasababishwa na ndugu na jamaa wa marehemu wanaposhindwa kuelewana.

"Kwa kawaida, sheria na taratibu zinazoongoza mirathi hazina tatizo, tatizo linakuja pale ndugu na jamaa wa marehemu wanaposhindwa kuelewana katika vikao vyao vya familia na ukoo," alisema. Alifafanua kuwa kuchelewa kukamilika kwa mirathi huwanyima warithi manufaa yao chini ya mirathi, hivyo akataka kikao hicho kije na mapendekezo juu ya namna bora ya kumaliza tatizo hilo ambalo mawakili wametajwa pia kuchangia kuchelewesha mirathi.

Aliwataka wadau hao kutambua kuwa mashauri yote ya madai na ucheleweshwaji wa mashauri hayo hausababishwi zaidi na upungufu wa sheria, bali udhaifu wa wasimamizi wa utoaji haki na wateja.

"Maahirisho marefu yasiyokuwa na sababu za msingi na mapingamizi yasiyo ya lazima, ni miongoni mwa sababu kuu za ucheleweshwaji wa mashauri, na kwa kuwa hiki ni kikao cha wadau muhimu wa haki, ni matarajio yangu kuwa mtakuja na maazimio ya namna bora ya kumaliza tatizo hili," alisema.

Profesa Ibrahim alisema ili kamati hiyo itekeleze majukumu yake kwa mafanikio, ni lazima ijiulize na kujibu swali la umuhimu wa mashauri ya madai kwa maendeleo ya nchi.

"Malengo makuu ya serikali ni kuiwezesha nchi yetu iliyoingia katika ya uchumi wa kati mwezi Julai mwaka huu, kupanda zaidi. Azma hii imeelezwa sehemu mbalimbali kama vile katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inayolenga kuwa na uchumi imara wenye ushindani," alisema.



Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na masuala ya wanawake (UN WOMEN), Hodan Addouh (kulia), akimsikiliza Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Dorothy Gwajima (kushoto) pamoja na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, (katikati) jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ruksa hati ardhi kwa wanandoa wote

**Na Waandishi Wetu,** SIHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema ni ruksa hati ya ardhi kuandikwa zaidi ya jina moja na kwamba wanandoa pia wanaweza kufanya hivyo.

Lukuvi alisema hilo jana mjini hapa wakati wa kutoa uamuzi juu ya mgogoro wa shamba la Kirari kati ya wananchi wa Kijiji cha Mlangoni na Watawa wa Kanisa Katoliki, uliodumu kwa zaidi ya miaka 40.

Alikuwa akifafanua taarifa zilizokuwa zimetanda kwenye mitandao ya kijamii kuwa wanandoa wanaruhusiwa kuwa na hati ya pamoja ya umiliki wa ardhi, tofauti na ilivyo kuwa zamani.

Waziri Lukuvi alisema wizara yake inakubali kusajili majina zaidi ya moja yakiwamo ya wenza katika hati za ardhi ili kuepusha matatizo ya mirathi baadaye. Alisema hiyo ni fursa kwa wanawake kushawishi waume zao katika kutekeleza suala hilo kwa kuwa sheria iko wazi na hakuna ofisa ardhi atakayehoji suala hilo.

Alisema hata mtoto chini ya miaka 18 anaweza kusajiliwa katika hati kwa masharti kuandikwa pia jina la msimamizi.

"Kinamama mna ushawishi mkubwa, washawishini waume zenu waandike majina mawili ili kuepuka mgogoro hata kama una mke zaidi ya mmoja," alisisitiza.

Aidha, Waziri Lukuvi alisuluhisha mgogoro uliodumu kwa takriban miaka 40 ambao ulileta uhasama na chuki baina ya Shirika la Watawa wa Kanisa Katoliki na wananchi wa kijiji cha Mlangoni, Siha mkoani wa Kilimanjaro kuhusiana na shamba la Kirari.

Katika shamba hilo, wananchi wanaioshi eneo lenye ukubwa wa ekari 347 na Watawa kubakia na ekari 1,063 ambapo kwa mara ya kwanza hati ya shamba hilo ilitolewa tarehe Oktoba 26, 1950 kwa ajili ya shughuli za ufugaji na kilimo.

Lukuvi alifikia hatua hiyo na pande hizo mbili baada ya kukutana na viongozi wa kijiji na watawa hao kwa lengo la kutafuta suluhu baada ya Mahakama ya Rufania Tanzania kuwapatia ushindi watawa, hivyo kulazimu wananchi wanaokadiriwa kuwa 3,700 kutakiwa kuondoka katika shamba la Kirari.

Waziri alifika katika kitongoji cha Kirari jana akiwa katika ziara yake ya kutembelea wilaya za Hai na Same mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya ardhi.

Katika mkutano wake na wananchi na watawa, Lukuvi alisema katika kutafuta suluhu ya mgogoro wa eneo hilo lilokuwa limegawanywa katika hati mbili, moja ikiwa na ekari 347 na nyingine ekari 1,063, serikali iliamua kuingilia kati mgogoro huo ili kunusuru nyumba 268 kuondoshwa katika eneo hilo.

"Hatukuingilia wala hatupingani na hukumu ya Mahakama ya Rufani, bali tumekuja ili watawa wapate haki yao kwa njia tofauti, hii ni 'win win situation'," alisema.

Kwa mujibu wa Lukuvi, baada ya serikali kufanya mazungumzo na watawa kuhusu suluhu ya mgogoro huo, Shirika la Watawa wa Kanisa Katoliki lilikubali kuachia sehemu ya maeneo yaliyovamiwa kwa lengo la kurudishiwa thamani ya eneo husika kwa gharama za serikali.

Katika ufumbuzi wa mgogoro huo, mbali na wavamizi kuamuliwa kulilipa shirika la watawa kwa kurudishiwa thamani ya eneo husika, pia shirika hilo limekubali kulipa fidia kwa nyumba 10 zilizokuwa karibu na shirika la watawa ili kuepuka mwingiliano.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alisema, wananchi waliovamia shamba hilo watamilikishwa kwa hati hawatalipa tozo ya mbele (premium) bali watalipa thamani ya ardhi pamoja na fedha ya kumilikishwa na kusisitiza kuwa eneo hilo limetengewa pia maeneo ya barabara, soko, kuzikia, shule na ofisi ya kijiji.

Kwa mujibu wa Lukuvi, watawa wamekubali kupoteza kidogo na kukubali wananchi wabaki kwa masharti ya kufidia thamani ya ardhi waliyoachiwa kwa kuwa kubomoa nyumba za wananchi ni gharama kubwa na kusisitiza fidia italipwa kwa viwango vya serikali.

■**Imeandikwa na Munir Shemweta, Mary Mosha.**

# Mitambo ya Symbion kunadiwa kulipa mishahara wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Kazi, imeamuru Kampuni ya kufua umeme Symbion Power Tanzania Limited, kuwalipa waliokuwa wafanyakazi wake zaidi ya Sh. bilioni 12 ambazo ni malimbikizo ya mishahara yao.

Wafanyakazi hao 43, wanaidai kampuni hiyo Sh. 12,249,890,439 tangu mwajiri huyo aliposimama kuwalipa mwaka 2016 baada ya serikali kupitia Shirika la Umeme (TANESCO) kusitisha mkataba.

Hata hivyo, kutokana na kampuni hiyo kutokufanya kazi, imeamuriwa kuwa mitambo ya kampuni hiyo ipigwe mnada na fedha zitakazopatikana zitumike kuwalipa fidia wafanyakazi hao. Katika uamuzi wa shauri Na. 60 la mwaka 2019, ulitolewa Novemba 13, mwaka huu na gazeti hili limeona nakala yake, Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, Warsha Ng'humbu, alisema mawakili wa upande wa wadai na mjibu maombi, hawakuwa na pingamizi lolote juu ya jambo hilo hivyo kuamuru wafanyakazi hao kulipwa haki zao.

Ng'humbu alisema awali, wafanyakazi hao waliungana na mwenzao, Maganga Kadogosa ambaye aliwasilisha kesi kudai kulipwa malimbikizo ya Sh. milioni 24 za mishahara yake. Kutokana na kushinda shauri hilo, wafanyakazi hao, wakiwakilishwa na Alex Kisinga, waliungana na kufungua shauri hilo nao wakitaka kulipwa malimbikizo yao ya mishahara.

"Shauri hili lilifunguliwa na Maganga Kadogosa ambaye aliomba mahakama kutoa amri ya kulipwa kwa malimbikizo yake ya mishahara yaliyofikia Sh. 24,000,000. Kwa kuwa wafanyakazi hao walithibitishwa kama ilivyokuwa kwa Kadogosa kuwa walikuwa wafanyakazi wa mjibu maombi, mahakama iliwaunganisha katika shauri la madai wakiliwakilishwa na Alex Kisinga.

"Kutokana na pande zote zikiwakilishwa na Mary Awe (mleta maombi) kupitia Kamishna wa Kazi na Makene Emmanuel upande wa mjibu maombi kutokuwa na pingamizi, mahakama inatoa amri ya wafanyakazi hawa 43 kulipwa jumla ya Sh. 12,249,890,439 kama kiasi cha kila mmoja kilivyoonyeshwa katika karatasi la madai ya malimbikizo yao," alisema Naibu Msajili katika uamuzi huo. Mmoja wa maofisa wa kampuni ya Udalali ya Kishe Auction Mart, iliyopewa kazi ya kunadi mitambo na mali za Symbion, ambaye hakutaka kutajwa jina lake kwa vile siyo msemaji wa mahakama, alikiri kupata amri ya mahakama.

Hata hivyo, alisema mchakato wa kunadi mitambo hiyo bado haujaanza kwa sababu kuna hatua mbalimbali za kufuata kisheria mpaka kufikia hatua hiyo.

HABARI KITAIFA

# Ma-RC, ma-DC wanavyohaha ujenzi wa madarasa

**Na Waandishi Wetu**

WAKUU wa mikoa na wilaya wameanza kutekeleza agizo la ujenzi wa madarasa kwa ajili ya wanafunzi waliokosa nafasi za kujiunga na kidato cha kwanza mwakani licha ya kufaulu.

Zaidi ya wahitimu 74,000 wa darasa la saba mwaka huu, hawajachaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Tayari serikali imeshawaagiza wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi kuhakikisha vyumba vya madarasa zaidi ya 1,000 vinajengwa kufikia Februari 28 mwakani.

Katika utekelezaji wa agizo hilo la serikali, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amewaagiza viongozi wa ngazi zote mkoani mwake kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu, wanajiunga na kidato cha kwanza mwaka ujao.

Akizungumza katika kikao cha kutangaza matokeo ya darasa la saba mkoani Kilimanjaro jana, Dk. Mghwira alisema wamebaini kuna upungufu wa madarasa 60 kwa ajili ya kutumiwa na wanafunzi 3,100 kwa mkoa mzima.

"Nimepokea taarifa kuna upungufu wa madarasa, Same ni madarasa 28, Hai madarasa 18, Siha madarasa saba na Moshi saba. Hakikisheni hii haiwi sababu ya wanafunzi kushindwa kuingia darasani kwani mnapaswa kuleta mipango mikakati yenu ambayo mmeiweka toka mlipopata matokeo.

"Viongozi wote hakikisheni wanafunzi waliohitimu darasa la saba 2020, wanajiunga na kidato cha kwanza 2021 na kwa mtu yeyote atakayesababisha wanafunzi wasiripoti kidato cha kwanza, achukuliwe hatua za kisheria," aliagiza.

Alizitaka halmashauri kuhakikisha zinatatua tatizo la uhaba wa madarasa kwa shule zote kwa kukaa na wataalamu kuona namna ambavyo wanafunzi watakavyoendelea kutumia mabwalo au kuingia kwa ratiba ya kuachiana darasani wakati ujenzi wa madarasa ukiendelea.

Ofisa Elimu Mkoa wa Kilimanjaro, Paulina Mkwama, alisema katika mkoa huo, kulikuwa na watahiniwa 34,744 na waliofaulu ni 30,834, sawa na asilimia 88.84 ikiwa ni ongezeko la asilimia moja kulinganisha na matokeo ya mwaka 2019.

Wakati hali ikiwa hivyo Kilimanjaro, wilayani Muheza, mkoani Tanga, kumetolewa agizo kwa maofisa watendaji wa kata, vijiji, maofisa tarafa, waratibu wa elimu kata, wakuu wa idara na madiwani kuanzisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari.

Jana, Mkuu wa Wilaya hiyo, Mwanasha Tumbo, aliwaagiza watendaji hao kuwahamasisha wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo kujitolea nguvu zao kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Alisema hataki kusikia mtoto ameshindwa kwenda shule kusoma kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati .

Mkoani Shinyanga, wanafunzi 234 waliofaulu kujiunga na sekondari mwakani wamekosa nafasi kutokana na tatizo hilo hilo la uhaba wa vyumba vya madarasa.

Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, alisema juzi kuwa katika mkoa huo, wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa la saba mwaka huu ni 33,435 na waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza ni 26,382.

"Wanafunzi hawa 234 ambao wamekosa shule, watajiunga na masomo haya ya kidato cha kwanza pale ujenzi wa vyumba vya madarasa utakapokamilika, mkoa umejipanga hadi kufikia Januari 28 tatizo hili liwe limeshatatuliwa," alisema Msovela.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Shinyanga, Mohamed Kahundi, alisema mkoa huo una upungufu wa vyumba vya madarasa 5,881 na madawati 16,672.

Kwa miaka mitatu mfululizo, ripoti za ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zimekuwa zikionyesha nchi inakabiliwa na uhaba wa samani na miundombinu katika shule zake.

**●Imeandikwa na Mary Mosha (MOSHI), Steven William (MUHEZA) na Marco Maduhu (Shinyanga).**

# Majaliwa achukizwa bandari kutofanya kazi miaka mitatu

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa (pichani) ameipa wiki mbili kuanzia juzi Mamlaka ya Bandari (TPA) ihakikishe ifikapo Januari Mosi, mwakani, Bandari ya Kimkakati ya Kagunga iliyoko Kata ya Kagunga wilayani Kigoma iwe imeanza kutoa huduma.

"Leo (juzi), nimekuja hapa kuona bandari, hii bandari ilikamilika mwaka 2017 imekaa tu, nyumba zimejaa popo tu na mle ndani kumejaa takataka na mmefagia jana baada ya kusikia mimi ninakuja.

"Ovyo kabisa, ninawauliza hapa wanajikanyaga tu, tuna mtumishi hapa? Hakuna mtumishi, alikuja jana baada ya kusikia ninakuja, ovyo kabisa hawa," alifoka.

Kiongozi huyo wa serikali alitoa agizo hilo baada ya kukagua mradi wa Bandari ya Kagunga iliyoko kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Waziri Mkuu alisema mbali na bandari hiyo kuanza kazi Januari Mosi mwakani, pia ameagiza soko la kisasa la Kagunga nalo lianze kazi siku hiyo hiyo ili kuwawezesha wananchi wa Kagunga kufanya biashara na kuinua kipato chao.

Waziri Mkuu pia alishangazwa na kuchukizwa na kitendo cha Meneja wa Bandari kutoka Makao Makuu ya TPA ambaye hajawahi kufika katika bandari hiyo na haijui.

"Kama kweli wewe ni Meneja wa Bandari Tanzania, bandari zako huzijui na una miaka chungu nzima, unafanya kazi gani? Ovyo kabisa," Majaliwa alifoka.

Waziri Mkuu alisema mradi wa ujenzi wa bandari hiyo ulikamilika mwaka 2017 ukihusisha ujenzi wa jengo la abiria na la mizigo, nyumba ya kuishi mtumishi na jengo maalum lakini hakuna mtumishi katika bandari hiyo ambayo ujenzi wake uligharimu Sh. bilioni 3.8.

"Tarehe moja ya mwezi wa kwanza mwaka 2021, ninataka bandari hii ianze kazi, nenda mkajipange. Hapa hakuna mtumishi, hamisha watumishi kama wapo Dar es Salaam, kama wapo Kigoma leta watumishi hapa wawatumikie wananchi kwenye bandari hii," aliagiza.

Aliwaagiza watendaji wa TPA kuruhusu meli na boti za watu binafsi zifanye kazi ya kutoa huduma katika bandari hiyo ili kuwawezesha wananchi kusafiri na kusafirisha mizigo kwa urahisi. Alisema serikali inataka majengo hayo yatumike kama ilivyokusudiwa.

"Hizi fedha za Watanzania, Sh. bilioni 3.8 watu wanafanya nazo mchezo tu, ninataka nione bandari hii inafanya kazi," aliagiza.

Pia, Waziri Mkuu aliwataka raia wa Burundi wanaohitaji kuingia nchini, wahakikishe wanafuata taratibu zote za uhamiaji kabla ya kuingia nchini.

"Sisi Tanzania na Burundi ni ndugu, ili kudumisha amani na kuimarisha ujirani mwema, kila mmoja afuate sheria na taratibu zilizopo," Majaliwa aliagiza.

Waziri Mkuu pia alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kigoma, Pendo Mangali, kuhakikisha anashughulikia madai ya vijana waliokuwa wanafanya kazi za vibarua katika ujenzi wa miradi hiyo ya maendeleo wanalipwa stahiki zao.



"Mkurugenzi hapa lazima uje tena, kajipange Jumatatu tarehe 21, Desemba, uje hapa ukutane na walalamikaji wote, uratibu mzuri uwekwe ili hawa wapate haki zao na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya simamia hawa vijana wapate stahili yao," aliagiza.

Waziri Mkuu yuko mkoani Kigoma kwa ziara ya kikazi ya siku mbili.

## Mahakama yataifisha almasi ya bilioni 62/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imeamuru madini ya almasi yenye uzito wa Carats 7,654.45 yaliyokamatwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere yakisafirishwa kwenda Ubelgiji, wenye thamani ya Sh. bilioni 61.97 kuwa mali ya serikali.

Madini hayo yalikamatwa wakati yakisafirishwa na vigogo wawili akiwamo Mkurugenzi wa Uthaminishaji Almasi na Vito Tanzania (TANSORT), Archard Kakugendo na Mthamini Almas wa Serikali, Edward Rweyemamu.

Mbali na kutaifisha madini hayo, mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Godfrey Isaya, imewahukumu vigogo hao kulipa faini ya Sh. milioni moja kila mmoja au kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka mitatu, baada ya kufanya makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na kukiri makosa yao.

Mahakama hiyo pia iliwatia hatiani kwa kosa la kuisababishia serikali hasara Sh. bilioni 61.9.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa juzi, Wakili wa Serikali Mkuu, Monica Mbogo, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wake umekamilika na kwamba DPP ametoa kibali iendelee kusikilizwa na Mahakama ya Kisutu.

Wakili wa Serikali, Jaqline Nyantori, alidai kuwa washtakiwa wote wanakabiliwa na shitaka la kuisababishia serikali hasara kwamba Agosti 25 na 31, 2017, mahali tofauti Dar es Salaam na Shinyanga, kwa pamoja wakiwa wathamini wa Wizara ya Nishati na Madini, walisababisha hasara ya Dola za Marekani 29,509,821.84 (Sh. bilioni 61.9).

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, aliomba mahakama kupokea kielelezo hicho cha madini kama ushahidi ambapo kilipokewa na washtakiwa walitiwa hatiani kama walivyoshtakiwa.

Nyantori aliomba mahakama itoe amri ya kutaifisha madini hayo kuwa mali ya serikali na washtakiwa wapewe adhabu kama mahakama itakavyopanga ili iwe fundisho kwa wengine ambao wanataka kuihujumu nchi kwa kutorosha madini.

Mshtakiwa Kalugendo kabla ya kutolewa kwa adhabu, aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa amekaa mahabusu miaka mitatu na amefanya kazi wizarani huko kwa miaka 22 na hakuwahi kukosea zaidi ya kosa hilo alilodai la kwanza.

Mshtakiwa wa pili, Rweyemamu pia aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ni kosa lake la kwanza na amefanya kazi wizara hiyo kwa miaka 22, hivyo mahakama imwonee huruma.

Hakimu Isaya baada ya kusikiliza pande zote mbili, aliwahukumu kulipa faini ya Sh. milioni moja kila mmoja au kwenda jela miaka mitatu na kutoa amri ya kutaifisha madini hayo kuwa mali ya serikali.

Washtakiwa walifanikiwa kulipa faini na waliachiwa huru.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa walikuwa wanakabiliwa na kesi ya kuisababishia serikali hasara ya Sh. 2,486,397,982.54 kati ya Agosti 25 na 31, 2017 wakiwa Dar es Salaam na Shinyanga.

# Wanaougua uti wa mgongo waomba kukumbukwa ajira

**Na Somoe Ng'itu**

TAASISI ya Watu Wanaougua Uti wa Mgongo (KASI), imeomba kundi hilo likumbukwe fursa za ajira zinapotokea nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa KASI, Abdulazizi Shambe, alipopokea msaada wa vifaa mbalimbali na fedha taslimu kutoka kampuni ya michezo ya kubahatisha Meridian.

Alisema taasisi yao ina wanachama 1,300 nchini na miongoni mwao wapo vijana wasomi wenye uwezo wa kuajiriwa, lakini wengi wao wanakutana na vikwazo vya kukubalika kila wanapoomba ajira.

"Tunao madereva, walimu, waandishi wa habari na hata mimi nina leseni B ya ukocha ya UEFA ambayo nilisoma Sweden mwaka 2001 hadi 2003 kabla ya kuugua.

"Mkurugenzi wetu taifa (Goodwill Linus) ana digrii ya uandishi wa habari, mzee wetu kwenye taasisi, Mohammed Tega ni dereva mzuri wa malori, ila wapo wengi wenye taaluma mbalimbali ingawa wachache sana ndiyo wanapata ajira akiwamo mwalimu Furaha Mbilinyi anayefundisha Shule ya Msingi Lugalo," alisema.

Kiongozi huyo alisema wamekuwa wakikabiliwa na vikwazo vingi kutoka kwa baadhi ya waajiri wanaoshindwa kuwapa ajira watu wenye tatizo hilo wakihofia namna ya kuwahudumia.

Alisema kuwa wanapokuwa kazini, jambo ambalo waajiri hawalifahamu ni kwamba wakiingia eneo la kazi hawatoki hadi muda wa kazi uishe.

"Hiyo ni faida ambayo waajiri wengi hawaielewi wanapoajiri mtu anayeugua uti wa mgongo," alisema huku akiwashukuru Meridian Bet kwa msaada wao aliouelezea kuwa umewapa faraja na kuona bado kuna jamii inawakumbuka watu wenye tatizo hilo.

Kampuni hiyo iliwakabidhi vyakula mbalimbali ikiwa unga, sukari, mafuta na vitu vingine vya mahitaji ya kibinadamu na pesa taslimu kwa ajili ya kuendeleza taasisi hiyo iliyoanzishwa mwaka 1991 na kusajiliwa mwaka 1997.

Meneja uendeshaji mwandamizi wa Meridian Bet, Carlo Njatu, alisema wametoa mkono wa faraja kwenye taasisi hiyo ili kuwafariji na kuendelea kusaidia jitihada za taasisi hiyo kama ambavyo sera ya kampuni yao inataka.

"Meridian Bet imekuwa ikishiriki katika kusaidia jamii pia, ukiachana na kazi ambazo imekuwa ikifanya za michezo ya kubashiri, imekuwa ikirudisha kwa jamii na kutoa mkono wa faraja kwa wahitaji," alisema.

Alisema mwaka huu wametoa misaada mbalimbali ikiwamo kusaidia hospitali ya wazee Kinyerezi, wagonjwa wa kansa wanaotibiwa Ocean Road, watu wenye ualbino Kigamboni, waathirika wa dawa za kulevya Kigamboni, kushiriki kusaidia upimaji macho bure na kutoa miwani kwa waliotakiwa kutumia jijini Dar es Salaam.



Ofisa Mradi wa Vodacom Tanzania Foundation, Salome Mtali (kushoto), akitoa maelezo kwa wanafunzi wa shule mbalimbali za sekondari kuhusu namna ya kujiunga na huduma ya Instant School, inayomwezesha mwanafunzi kupata masomo mbalimbali Kidijitali bure kupitia mtandao wa Vodacom, wakati wa tamasha la utoaji wa Tuzo za Uwezo 2020, zilizoandaliwa na Taasisi ya Great Hope Foundation, lililofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wauguzi wachunguzwa tuhuma kuuza dawa na kupokea rushwa

**Na Neema Hussein,** KATAVI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Katavi, inachunguza tuhuma za wizi wa dawa, kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wagonjwa zinazowakabili watoa huduma watatu wa Kituo cha Afya Ilembo, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Katavi, Christopher Nakua, alisema jana kuwa Hussein Hassan, mmoja wa wauguzi hao, anadaiwa kukamatwa akiwa na begi lenye dawa za binadamu alizokuwa akiwauzia wagonjwa kwenye wodi ya wazazi nyakati za usiku.

"Hussein Hassan, muuguzi kwenye wodi ya wazazi alikamatwa Desemba 14 mwaka huu na baada ya kuanza kuhojiwa na uongozi wa kituo hicho na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, alikiri kutenda kosa hilo lakini alikimbia kwa lengo la kujaribu kutoroka na aliacha pikipiki yake," Nakua alidai.

Alisema muuguzi wa pili ni Charles Daniel aliyekuwa kwenye wodi ya wazazi katika kituo hicho ambaye anadaiwa kuomba rushwa kwa mume wa mgonjwa aliyekuwa amelazwa katika kituo hicho.

"Tarehe 13 Desemba mwaka huu, majira ya saa mbili usiku, aliomba rushwa ya Sh. 20,000, lakini alipewa Sh. 10,000 na mume wa mgonjwa huyo ili amsaidie mgonjwa wake kujifungua salama," alidai.

Nakua alisema uchunguzi wa awali umeonyesha kuwa baada ya muuguzi huyo kubanwa na Muuguzi Mfawidhi na Kaimu Mganga Mkuu wa Kituo hicho, alirudisha fedha Sh. 10,000 kwa mhusika.

Alisema muuguzi wa tatu, Isack Muhigi anakuwa kuwa Desemba 13 mwaka huu, majira ya mchana alimwomba mgonjwa rushwa ya Sh. 10,000 na kupokea fedha hiyo ili amsaidie kupatiwa huduma ya kujifungua salama na kwamba baada ya kubanwa, alimrudishia mgonjwa huyo fedha mbele ya Kaimu Mganga Mkuu wa Kituo hicho.

Alisema taasisi hiyo inaendelea na uchunguzi wa tuhuma hizo na pindi utakapokamilika na kuthibitika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani, akiupongeza uongozi wa kituo hicho kwa ushirikiano katika kupambana na vitendo vya rushwa.

Alitoa wito kwa watumishi wa umma mkoani hapa na jamii kwa ujumla, kutojihusisha na vitendo vya jinai kama kuomba na kupokea rushwa pamoja na kuiba vifaa vya serikali.

# RC apiga 'stop' madalali kupewa vizimba

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, amepiga marufuku baadhi ya masoko kupangisha vizimba kwa madalali kisha watu hao kuwapangishia wananchi kwa bei ya juu.

Amesema jambo linalowaumiza wafanyabiashara wakati lengo la serikali kujenga masoko hayo ni kuwasaidia wafanyabiashara na si kuwakandamiza.

Kunenge alitoa onyo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati wa ziara yake ya kikazi na kuwaagiza wakurugenzi wa manispaa zote kukaa pamoja na kufanya mapitio ya bei elekezi za kupanga kwenye masoko ili kusiwe na kupishana kwa gharama za upangaji.

Alisema masoko yanayojengwa yakikamilika na wafanyabiashara wakapangiwa sehemu za kuuza bidhaa zao, ni marufuku kwa mfanyabiashara kufanyabiashara nje ya masoko au sehemu zisizo rasmi.

Akiwa kwenye Mradi wa Soko la Tandale, alimtaka mkandarasi kukamilisha kazi ifikapo Aprili, mwakani kutokana na umuhimu mkubwa wa soko hilo.

Pia akiitaka kampuni ya MECCO inayojenga soko la Kibada kwa gharama za Sh. bilioni 6.6 naye kuhakikisha anakamilisha kabla ya Mei ili wananchi wanufaike na manispaa ipate mapato.

Kunenge pia alitembelea Mradi wa Ujenzi wa Barabara tano zenye urefu wa kilomita 10.5 za muungano chini ya DMDP na kukasirishwa na kusuasua kwa mradi huo huku wahusika wakitoa kisingizio cha corona na mvua

Alimtaka mkandarasi, Kampuni ya CRJE kufanya kazi usiku na mchana na kukabidhi mradi mwishoni mwa Januari pasipo kisingizio chochote.

Pia alitembelea barabara ya Mikadi Beach Sheraton yenye urefu wa mita 800 inayotekelezwa na mkandarasi kutoka Osaka Ltd na ujenzi wa daraja la Malimbika linalounganisha Kata ya Somangila na Kisarawe II chini ya Lumo Cons Ltd na kuwataka makandarasi kukamilisha miradi kwa wakati.

# Pangani kicheko kupata huduma ya X-Ray

**Na Steven William,** PANGANI

SERIKALI imepeleka mashine ya kisasa X-Ray katika Hospitali ya Wilaya ya Pangani mkoani Tanga kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi ambao walikosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

Mbunge wa Pangani na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema jana kuwa serikali imepeleka mashine hiyo, hivyo kuondoa kero iliyokuwa ya muda mrefu kwa wananchi kutokana na kukosa huduma hiyo.

Alisema kutokana na ukosefu wa huduma hizo, wananchi walikuwa wanafunga safari kufuata huduma ya X-Ray Tanga mjini umbali wa kilomita 50. Hali hiyo alisema wananchi wa hali ya chini kiuchumi, hususani wazee na kinamama, walikuwa wanashindwa gharama ya fedha ya usafiri.

Baada ya kuona wananchi wanapata shida kukosa huduma hiyo, alisema alianza kazi ya kupigania serikalini na hatimaye imepatikana, sasa wananchi wa vijijini na mjini wanapata huduma kwa raha.

Alisema kuwa mashine hiyo ya kisasa kubwa imeletwa katika hospitali ya wilaya na imeanza kazi rasmi wananchi wanapata huduma bora. Aliahidi kuboresha hospitali hiyo kwa kupigania kuongeza vifaa tiba na dawa ili wananchi wapate huduma bora na nafuu.

Waziri alimwagiza mganga mkuu wa Wilaya ya Pangani kuhakikisha X-Ray hiyo inatumika kama ilivyokusudiwa kutoa huduma kwa wananchi na si kuiweka stoo ikawa nyumba ya panya hapo hawataelewana watazinguana hataki mchezo wananchi wake wapate tabu.

Halima Selemani, mkazi wa Kata ya Bushiri, alisema wanamshukuru mbunge kwa kupigania kupatikana kwa huduma hiyo katika hospitali ya wilaya kwa kuwa kinamama na wazee walikuwa wanapata shida kufuata huduma hiyo Tanga mjini.

Naye Juma Athumani, mkazi wa Pangani mjini, alisema mbunge huyo amefanya jambo kubwa na imesaidia kupata huduma kwa kuwa watu waliokuwa wanafunga safari kwenda Hospitali ya Rufani ya Bombo, jijini Tanga.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, Akida Bahorera, alisema mashine hiyo itasaidia kutoa huduma bora na za kisasa na kuwataka watumishi kuitunza idumu muda mrefu.

Kwa upande wake, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Pangani, Mohamed Moyo, alisema serikali kuleta mashine hiyo, ni utekelezaji wa serikali katika utoaji wa huduma bora kama ilivyoainishwa katika ilani ya CCM.

## Jafo akerwa viongozi kubeza 'Force Account'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Selemani Jafo, amekerwa na baadhi ya viongozi wa serikali wanaobeza matumizi ya mfumo wa 'Force Account' katika utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Jafo alibainisha hayo jana alipotembelea na kukagua ujenzi wa mradi wa Hospitali ya Uhuru jijini hapa ambao umekamilika kwa asilimia 99. Alisema mfumo wa Force Account umekuwa mkombozi hasa katika kuokoa kiasi kikubwa cha fedha za miradi mbalimbali iliyotekelezwa na serikali. Alisema mfumo huo ndiyo huwa unamwelekeza mtu akienda eneo la mradi anapata kitu kwa bei fulani huku akieleza kushangazwa na baadhi ya viongozi hao wa serikali wanaokashifu utaratibu huo.

"Zamani, jengo kama hili tulikuwa tunajenga kwa Sh. bilioni 10 hadi 20, lakini leo kwa thamani ndogo, halafu unakuta viongozi wengine wanasimama jukwaani wanakashifu 'Force Account'," alisema.

Jafo alisema lengo la Rais John Magufuli ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya kupitia hospitali hiyo na nyinginezo zilizojengwa mkoani hapa.

Alibainisha kuwa katika uongozi wa Rais Magufuli, wamejenga kwa kutumia mfumo huo vituo vya afya 487 na kwamba awali kwa kutumia wakandarasi, majengo kama hayo yalikuwa yanajengwa kwa gharama kubwa. "Ninaomba viongozi wenzangu wengine mnaokaa mnakashifu utaratibu wa 'Force Account', msiongopewe, hivi hamfikiri zamani jengo la Sh. bilioni mbili leo linajengwa kwa Sh. milioni 500?

"Halafu leo watu wanasimama wanasema utaratibu huu hauna maana, unajua kuna watu wa ajabu sana na inawezekana wengine hawajui maisha halisi ya Watanzania, huu utaratibu umetusaidia shule kongwe zimekarabatiwa," alifafanua Jafo.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binillith Mahenge, alisema mradi huo haujakamilika kutokana na kutotolewa kwa kiasi cha fedha kinachohitajika. "Fedha zilizotolewa bado hazitoshi maana kuna zilizoongozeka za ujenzi wa barabara na ununuzi wa vifaa, hivyo tunaomba utusaidie zitoke tumalizie ujenzi huu," alisema Dk. Mahenge. Akitoa taarifa fupi ya umaliziaji jengo hilo tangu Waziri Mkuu afike Novemba 20, mwaka huu na kutoa maagizo, Mkandarasi kutoka Suma JKT, Girimu Kanansi, alisema mradi umekamilika kwa asilimia 99.

"Kwa upande wa rangi imekamilika kwa asilimia 99, vigae asilimia 99 maana kuna upungufu wa vigae vichache, mfumo wa maji taka asilimia 97, umeme asilimia 98, ambapo kuna upungufu wa baadhi ya taa, milango nayo inamaliziwa," alisema.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, akimkabidhi zawadi mwanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara, Ali Hemedi Ali, ambaye aliibuka mshindi wa jumla kwa ngazi ya Shahada ya Uzamili kwenye mahafali ya 55 ya chuo hicho, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

# Serikali yawapa somo wahitimu CBE

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewahimiza wahitimu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), kutumia elimu waliyoipata kujiajiri na kuajiri Watanzania wenzao badala ya kutembea na vyeti kutafuta ajira.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, katika mahafali ya 55 ya chuo hicho.

Alisema kuna fursa nyingi ambazo wahitimu wanaweza kuzitumia na kuwa na maisha mazuri wakiwa wabunifu kwa kuwa sekta binafsi ndiyo mwajiri mkuu na si serikali.

"Mimi ningetamani kusikia kila mmoja hapa anaanzisha kampuni yake. Wewe uliyesomea uhasibu anzisha kampuni ya kutengeneza hesabu za kampuni mbalimbali, uliyesomea ukaguzi anzisha kampuni ya kukagua hesabu na hata waliosomea masoko vivyo hivyo," alisema Mwambe.

Waziri alisema kazi ya serikali itakuwa kuweka mazingira mazuri kwa ukuaji wa sekta binafsi ili kuiwezesha kuongeza uzalishaji, kuongeza tija ili hatimaye Tanzania iwe na uchumi mkubwa Afrika Mashariki, Kusini mwa Afrika na duniani ikiwezekana.

Aliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa namna walivyomudu kukiongezea hadhi chuo hicho na kupanda kuwa miongoni mwa vyuo bora nchini kutoka nafasi ya 53 ndani ya miaka mitano hadi kuwa nafasi ya 14.

Alisema inawezekana kabisa Tanzania kuondokana na umaskini iwapo kila mmoja atawajibika na kuwa mbinifu kwenye eneo lake la kazi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo hicho, Esther Ishengoma, alisema kwa kuwa taifa linazalisha nafasi chache za ajira kuna uhitaji mkubwa sana wa kutengeneza nafasi hizo kwa kuzalisha wajasiriamali watakaojiajiri mara baada ya kuhitimu.

Alisema kwa kuzingatia hilo, CBE kwa kushirikiana na Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS), waliandika andiko la namna wanavyoweza kufanya kutatua tatizo la ajira nchini na kwamba wana imani wakiwa makini watalimaliza.

Vile vile, alisema chuo hicho kimekuwa kikisimamia vizuri mapato na matumizi yake kwa kuhakikisha kila fedha inayopatikana inatumika kama ilivyopangwa hali iliyosababisha wapate hati safi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kwenye manunuzi ya umma.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa kauli hii ya Waziri, mifuko hifadhi ya jamii sasa ibadilike

**KWA** muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wastaafu kuwa wamekuwa wakipigwa danadana na hata kukata tamaa wanapofuatilia malipo ya mafao yao kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Hatua hiyo imekuwa ikisababisha usumbufu mkubwa kwa wastaafu wengi ambao wamelitumikia taifa kwa muda mrefu na hata wengine kupoteza maisha wakiwa hawajapata fedha hizo ili kuendesha maisha yao baada ya utumishi kwenye sekta binafsi au serikalini.

Baadhi ya wastaafu ambao wengine wana takriban miaka miwili tangu kukoma kwa utumishi wao sasa, wameeleza kuwa wamekuwa wakihangaishwa na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa muda mrefu wakati wa kufuatilia mafao hayo. Hata wale walioachishwa ajira pia wameingia kwenye mkumbo huo wa kufuatilia mafao yao kwa muda bila mafanikio.

Miongoni mwa sababu ambazo zimekuwa zikitolewa na baadhi ya maofisa wa mafuko hiyo ni kukosekana kwa taarifa muhimu za wahusika kutoka kwa waajiri. Wastaafu na walioachishwa kazi, hasa kutoka sekta binafsi, huzungushwa na mifuko hiyo kwa madai kuwa waajiri hawakuwakilisha baadhi ya fedha za makato.

Sababu zinazotolewa na baadhi ya maofisa wa mifuko, ambao wamepewa dhamana ya kuwahudumia wastaafu na waliokosa ajira, zinaonyesha dhahiri kuwa kuna jambo lililojificha nyuma ya pazia. Kwa maneno mengine, huenda maofisa hao wanafanya hivyo ili kutoa mwanya wa kupata chochote kutoka kwa wastaafu.

Hata hivyo, baada ya kuwapo kwa kilio hicho cha wastaafu, angalau sasa kuna mwanga wa unafuu wa kutokuhenyeshwa juu ya mafao yao. Hali hiyo inatokana na serikali kuikemea mifuko hiyo na kuitaka kuacha ujanja ujanja na badala yake kuwalipa bila usumbufu wahusika fedha zao ambazo waliziwekeza kwa kukatwa kupitia mishahara yao na kiasi kingine cha fedha kutoka kwa waajiri.

Jambo la kufurahisha zaidi, serikali kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, imeonyesha sasa haina mzaha na mafao ya wastaafu.

Hatua hiyo inatokana na kauli aliyoitoa juzi ya kuwataka wakuu wa vyombo hivyo kuwachukulia hatua, ikiwamo kuwafukuza kazi kwa mujibu wa sheria, mameneja na wale wote wanaohusika kuchelewesha haki za watu hao.

Wakati akifunga semina ya viongozi wa Shirikisho la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Tanzania (TSSA), Mhagama licha kukerwa na ucheleweshaji huo, alionyesha kushangazwa na wafanyakazi wa mifuko ya hifadhi kuwadai barua za miaka 40 iliyopita wanachama wanaostaafu kama moja ya kielelezo.

Katika zama za sasa za sayansi na teknolojia, ni imani yetu kwamba mifuko ya jamii iko kidigitali, hivyo itakuwa na kanzidata zinazoonyesha maelezo ya kila mwanachama amebakiza muda fulani kustaafu.

Kwa mantiki hiyo, inapaswa kuwasiliana na waajiri wa wanachama hao kupata taarifa zile zinazokosekana kwenye kanzidata zao ili unapofika muda wa kustaafu, wahusika wasizungushwe kuhusu hali zao.

Ni wakati sasa, kama alivyosema waziri, mifuko ya jamii kubadilika na kuacha umangimeza kwa kufanya vitendo vilivyogubikwa na harufu ya rushwa kwa kuwafanya wanachama kusotea mafao yao na hata wengine kufariki dunia kabla ya kufaidi jasho lao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wavuvi wasirudi nyuma katika fursa hii kuboresha kazi zao



Na Sabato Kasika

**MIKOPO** ya kibiashara kutoka, katika benki ama taasisi rasmi za kifedha, ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya mitaji inayowezesha mfanyabiashara ama vikundi vya wafanyabiashara kuboresha shughuli zao.

Kutokana na umuhimu huo, halmashauri mbalimbali nchini zimekuwa zikihimiza uwezeshaji wa fedha za mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali vikiwamo vya wavuvi ili vijiletee maendeleo.

Wako vijana wengi wanaohitaji mikopo lakini bahati mbaya hawana dhamana za umiliki wa nyumba, mashamba au mali za thamani, hivyo kupitia vikundi wanaweza kukopesheka na kikundi kikawa ndicho dhamana ya mikopo.

Kikundi ni muunganiko wa watu, wasio ndugu wa karibu, ambao kwa hiari yao wameamua kujiunga na kuunda kikundi na wanafanana kwa makazi, mahitaji, malengo, shughuli au itikadi.

Njia ya watu kujiunga katika vikundi inaelezwa kuwa inarahisisha wao kupata mikopo ya halmashauri na hata kwenye taasisi za fedha ili kuboresha biashara na kujiletea manufaa zaidi.

Kwa kutambua hilo, wiki hii vikundi 79 vya wavuvi, vyenye wanachama 1,035 vya Wilaya ya Musoma mkoani Mara, vilijiandikisha kwa ajili ya kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha.

Vikundi hivyo vinaorodheshwa na maofisa wa Benki ya Equity katika ziara hiyo na sasa kinachoendelea ni maofisa hao kuonana na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, kujadili fursa ya upatikanaji wa mikopo kwa vikundi hivyo vya wavuvi.

Katika ziara hiyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii, Tanna Nyabange, anahimiza uanzishwaji wa vikundi ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi na pia kupata mikopo toka halmashauri ya Musoma na taasisi nyingine za fedha.

Ingawa kumekuwapo na tatizo kwa watu na hasa vijana kujiunga katika vikundi kutokana na sababu mbalimbali, jambo la muhimu ni wao kutambua fursa na kuzichangamkia ili kupanua wigo wa shughuli zao.

Serikali na taasisi zingine za fedha zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili ya mikopo ya biashara kwa vikundi mbalimbali ili kuyawezesha yajikwamue na umaskini, lakini baadhi hufa baada ya kupata fedha.

Kufa au kusambaratika kwa baadhi ya vikundi, kunaweza kusababishwa na kushindwa kusimamia malengo ya mkopo, hivyo wavuvi waliojiandikisha kwa ajili ya kupata mikopo walione hili ili lisiwakute. Lakini pia ni vyema elimu ikatolewa zaidi, isiwe ya siku moja tu kama hiyo iliyotolewa wakati wa kuhamasisha wavuvi kujiunga katika vikundi, kwa ajili kupata mikopo kutoka halmashauri ama taasisi za fedha.

Namna ya kupata fedha ni jambo la msingi kuliko yote katika shughuli za biashara, japo linaweza lisiwe jambo rahisi sana, kimsingi linaweza kuwa jambo gumu na la kukatisha tamaa wakati mwingine.

Hata hivyo, kama wavuvi watakuwa wameelimishwa na kujipanga vizuri, kupata fedha kwa ajili ya biashara zao, itakuwa rahisi kukopa na kuendesha shughuli zao na kurejesha mikopo kwa wakati.

Wavuvi wamethubutu, wameweza kujiandikisha kwa wingi kiasi hicho, kinachotakiwa sasa ni elimu ya kutosha ambayo itakuwa na faida kwao na kwa taasisi za fedha (kutokuwapo mikwaruzano).

Tayari vikundi hivyo vinafanya biashara ya uvuvi na sasa vinataka kuiboresha ili iwe na manufaa zaidi, hivyo msisitizo zaidi uwe katika elimu ambayo itavisaidia kuona mabadiliko baada ya kukopeshwa.

Mabadiliko hayo ni kuboresha maisha ya wavuvi na wanaweza kuwa na mchango katika kuongeza pato la serikali kupitia kodi zao, baada ya kuelimishwa na kupata mikopo na wa fedha ya kuitumia inavyotakiwa.

Serikali imewahi kusema, inatamani kuona uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya wafugaji na wavuvi kupitia mikopo inayotolewa na benki ikiwamo ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili kuyaongezea thamani mazao yanayotokana na sekta za mifugo na uvuvi.

Kwa hiyo kupitia mikopo, wavuvi waliojiandikisha ili kukopeshwa fedha, wanaweza kuendesha uvuvi huku wakiwa na viwanda vyao wenyewe vya kuchakata minofu ya samaki na kufaidika zaidi.

SAFU

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

> **Inaeleweka, kuwa tangu zamani viongozi walihitaji kusikia wananchi wao wanataka nini na walipata taarifa kupitia vyombo vya habari na mara moja walichukua hatua, na mrejesho ulirudi kwa wananchi kupitia njia hiyo hiyo.**

# Bashungwa karibu sekta ya habari lakini...

HIVI karibuni akiunda Serikali yake mpya ya kumalizia muhula wa pili wa Awamu ya Tano anayoiongoza, Rais John Magufuli, alimteua Innocent Bashungwa, kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Hii ni moja ya wizara nyeti katika nchi na inayofuatiliwa na wengi, kwanza kwa kuwa ndiyo inasimamia habari, lakini pia michezo na burudani zote. Hivyo kuwa na wafuasi wengi.

Bashungwa amechukua nafasi ya Dk Harrison Mwakyembe ambaye alitoa mchango wake kwa kipindi alichohudumu na kuondoka, kwa sababu zinazojulikana zihusuzo uchaguzi.

Waziri Bashungwa ni kijana, hivyo anastahili kuwa katika nafasi hiyo, na pia kongole kwa kuteuliwa tena kuwa Waziri, ambaye katika muhula wa kwanza alihudumu katika sekta ya biashara na viwanda.

Bila shaka Rais amemwamini, akijua kuwa ataitendea haki wizara hii, ambayo wanahabari na wadau wa habari wamekuwa wakiibebesha mzigo wa kusimamia mhimili wa nne (usio rasmi).

Umekuwa ukijulikana kama mhimili wa nne, baada ya Dola, Bunge na Mahakama, kutokana na mchango wake kwa jamii, na hakuna sekta ambayo imekuwa ikifanya wajibu wake, bila kuuhusisha mhimili huu. Wapo walioupenda, wapo waliouchukia.

Namshauri tu Bashungwa, asikae ofisini kusubiri taarifa za wasaidizi wake, atoke nje kama ambavyo Rais Magufuli amekuwa akisisitiza, akakutane na wadau awasikilize nini wanazungumza kuhusu wizara yake. Nampongeza ameshaanza, asiishie serikalini na chamani tu, afike hata vyombo binafsi, tena vyote.

Angalau katika michezo, Rais alishahadharisha kuwa anataka kuona timu za Taifa zinashinda mashindano yao na kutishia kumfuta kazi siku timu ya Taifa itakapoadhiriwa, lakini pia akasisitiza la wasanii kulindwa hasa katika maslahi yao.

Kwa upande wa habari, hayakuzungumzwa mengi, zaidi ya kuhimiza wanahabari kuendelea kuchapa kazi katika kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha, kama ilivyo dhima yao ya kila siku.

Bashungwa atakapokuwa anazunguka kuzungumza na wadau wa habari, kwa maana ya kampuni za habari, taasisi za kusimamia habari na wanahabari lakini na wananchi, ambao ndio wasomaji, watazamaji na wasikilizaji habari, afungue masikio sawasawa.

Si siri, kwamba tasnia ya habari leo, si kama ilivyokuwa huko nyuma. Vyombo vingi vya habari vimedorora kama si kufa au kuuawa. Habari za wananchi haziandikwi kama inavyofanyika kwa za viongozi.

Inaeleweka, kuwa tangu zamani viongozi walihitaji kusikia wananchi wao wanataka nini na walipata taarifa kupitia vyombo vya habari na mara moja walichukua hatua, na mrejesho ulirudi kwa wananchi kupitia njia hiyo hiyo.

Vyombo vya habari ni njia ya ukombozi wa mwananchi katika kuondokana na unyonge kimaisha, kwamba kupitia njia hiyo, ndipo uovu au matatizo huibuliwa na kuondolewa, na kumwezesha mwananchi kuzalisha mali bila matatizo wala malalamiko.

Tangu zamani, vyombo vya habari vilitumika kama njia ya ukombozi kisiasa duniani, na baada ya hapo vikatumika kuhamasisha uzalishaji mali katika kujikomboa kiuchumi. Hivyo vinapaswa kuendelea na jukumu hilo muhimu bila kunyamazishwa.

Kwa kuwa naamini Bashungwa analijua hili, atakuwa tayari kujipanga na wadau wake, kuhakikisha au kuwezesha wanahabari kufanya kazi yao ya msingi bila kutetereka, huku akiangalia uwezekano wa kuwasaidia kiuchumi.

Si siri, kwamba vyombo vingi kama si vyote, hususan binafsi, vina hali mbaya sana kiuchumi, hata kushindwa kujiendesha na hivyo kufungwa, na hiyo imetokana na kukosa matangazo ambayo awali yalikuwa injini za kiuchumi katika kampuni za habari.

Mtangazaji mkuu ambaye ni Serikali, ni kama amepunguza kunyoosha mkono wa kutangaza kama si kuukata kabisa, huku sekta binafsi ambayo nayo ilikuwa ikichangia, ikijikuta ikishindwa kukunjua mikono yake na kukosa kutangaza.

Kama hali hii itaendelea na mengine ambayo ni dhahiri Bashungwa atayasikia katika ziara zake kwenye vyombo vya habari, tutarajie kushiriki misiba ya vyombo vya habari kiasi wananchi wapate taarifa kupitia ama mitandao ya kijamii au nyimbo za wasanii. Serikali na sekta binafsi wakiungana, ukombozi utawezekana.

**Alamsiki!**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

> **Najua kabisa ni jukumu la mwajiri kufuatilia mwajiriwa wake na endapo ataharibu kazi, kuna stahiki yake ataipata. Lakini pia ni nani hivi sasa wakati huu ambao kazi au ajira ni shida, atachezea kazi? Nani atatoka kazini aende baa kunywa wakati kazi inamsubiri na kazi ndiyo inampa riziki?**

# Mitutu ya nini baa jamani?

NI saa saba mchana jua kali, joto kali. Niko katika moja ya baa maarufu katika kiunga maarufu cha Jiji la Dar es Salaam na rafiki yangu James.

James kaja kunitembelea akitoka nchi jirani, ambako anafanya kazi ya uandishi wa habari. Ananisimulia anavyoridhishwa na hali ya utulivu, lakini na ukarimu walionao Watanzania.

Baada ya kupata ugali na samaki, chakula anachokiri kukipenda sana, tunaendelea kubadilishana mawazo huku kila mmoja akinywa kinywaji anachokipendelea. Lakini si kinywaji baridi.

Wakati nikiendelea kumsimulia chanzo cha utulivu na amani nchini tofauti na kwao, na kumweleza kuwa ni matunda ya waasisi wa Taifa hili la Mwalimu Julius Nyerere, mara kwa nje linasimama gari rangi ya maziwa aina ya Toyota Land Cruiser la wazi.

Mara wanashuka watu takriban wanane, ambao wanajipambanua kuwa askari Polisi, kwani watatu wana bunduki aina ya SMG huku wengine waliosalia, wakiwa na pingu na wamevalia kiraia.

Kama kawaida ya polisi, wanaingia baa tuliyokaa kwa tambo na kukusanya vinywaji vya wateja, huku baadhi wakiwafunga pingu. Wakati nimepigwa butwaa nisijue la kufanya mbele ya mgeni wangu niliyemsimulia amani na utulivu, wateja wanaelekezwa kwenda kupanda lile gari na pingu zao.

Namsihi mgeni wangu atulie, huku nikivunga kuwa sijui kinachoendelea, lakini askari wawili wanasogelea meza yetu na mmoja ananiambia: "Mzee si unajua utii wa sheria bila shuruti? Mnakunywa pombe wakati si wake, haya garini."

Namwambia nimekuelewa ili nisisababishe mtafaruku ambao unaweza kumfanya mgeni wangu kubaki na taswira mbaya kichwani na kwenda kusimulia nyumbani kwao. Namfuata kiongozi wa askari hao garini, najieleza ananielewa, kwa nini tuko pale. Anatuacha twendelee. Namshukuru sana kwa kuwa ameniokoa kwa James.

Natumia fursa ile kumdanganya mgeni wangu kuwa kuna mhalifu wanamtafuta eneo lile lakini wamemkosa, na kauli ya pombe ni mbinu tu ya kuficha wanachokitafuta. Ananiamini lakini nabaki na siri moyoni.

Polisi wanatekeleza tamko lililotolewa na Serikali mwaka 2016 kuhusu kunywa pombe saa za kazi, likilenga kutekeleza kaulimbiu ya Hapa Kazi Tu. Natafakari kama tamko hilo bado lina mashiko hasa kwa wasio na kazi au kwa wenye kazi za zamu au binafsi.

Mtu analazimishwa kunywa pombe kwa kengele, kwamba ikifika saa 10 ndipo aanze kunywa, kwa kuwa wakati wa kazi ataathiri utendaji kazi. Najiuliza wa wapi, wakati kila mwenye kazi anajua alikoajiriwa na aina ya kazi anayoifanya.

Najua kabisa ni jukumu la mwajiri kufuatilia mwajiriwa wake na endapo ataharibu kazi, kuna stahiki yake ataipata. Lakini pia ni nani hivi sasa wakati huu ambao kazi au ajira ni shida, atachezea kazi? Nani atatoka kazini aende baa kunywa wakati kazi inamsubiri na kazi ndiyo inampa riziki?

Hivi bado kweli kuna haja ya kushurutishana kufanya kazi, wakati tukihubiriwa kuwa asiyefanya kazi na asile na asiyekula na afe, kweli? Kuna haja gani basi ya kushikiana mitutu baa, wakati mnywaji ananunua kwa pesa yake ambayo ndiyo pia huchangia pato la mmiliki wa baa, ambaye hatimaye hulipa kodi inayoongeza pato la nchi?

Watu wakiachiwa wanywe pombe saa 24/7 hatuoni kuwa ajira zitaongezeka na pato la nchi litaongezeka na hivyo miradi kutekelezwa? Kama kuna mwajiri anayeruhusu wafanyakazi wake kunywa au kulewa wakati wa kazi, bila shaka anajua anafidia vipi kipato chake.

Lakini kama mimi ni daktari, naingia kazini usiku na mchana nalala, na nina fedha zangu, nitakuwa nafanya dhambi gani kwenda baa kunywa wakati walio kazini wakiendelea kuwajibika? Je, kama mimi ni mstaafu nina fedha zangu, niko nyumbani saa 24/7, nikiamua kushinda au kukesha baa nikinywa, namkwaza nani?

Kama sheria zipo na zinaheshimika kwa maana hakuna mtu anayekwazika na unywaji wa mwingine, je sababu za kuzuia kunywa pombe saa za kazi tena nje ya eneo la kazi, bado zina mashiko katika kipindi hiki? Ni vema tukatafakari ili tusishikiane mabunduki baa.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Fitina hizi zinaiangamiza CCM Kyela



Na Thobias Mwanakatwe
mwanakatwe2015@gmail.com

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) ni chama kikongwe nchini ambacho kiliundwa mwaka 1977 baada ya kuunganishwa kwa vyama vya Tanganyika African National Union (TANU) cha iliyokuwa Tanganyika na Afro-Shiraz (ASP) cha Zanzibar.

Chama hiki kimejizolea umaarufu, heshima ndani na nje ya nchi hasa kutokana na kuendesha siasa za kistaarabu ambazo zimelifanya taifa kuwa na amani na utulivu wa kujivunia barani Afrika.

Kulingana na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila baada ya miaka mitano nchi hufanya uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani.

Kabla ya kuanza kwa kampeni ambazo ratiba yake hutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kila chama cha siasa kunachoshiriki uchaguzi husika huendesha kura za maoni kwa ajili ya kupata wagombea ambao hupambana na vyama vingine. CCM naweza kuweka wazi kwamba ni chama pekee ambacho kimekuwa kikiendesha mchakato wa kura za maoni kistaarabu.

Kwa utamaduni uliojengeka ndani ya chama na wanaCCM kwa ujumla ni kwamba baada ya kumalizika kura za maoni na kupatikana mgombea anayependekezwa na chama, makundi yote ya wanachama ambayo hujigawa kwa wagombea huvunjwa na kubaki kundi moja la CCM kwa ajili ya kumpigania mgombea aliyependekezwa na chama. Hata pale penye ushahidi wa uonevu kwa mgombea mmoja, CCM wamelelewa kumezea na hiyo ndiyo siri ya mafanikio ya chama hiki kikongwe.

Katika utaratibu huo, wakati wa kampeni za mgombea wa CCM ni nadra kusikia mgombea aliyependekezwa na chama kuanza kuwaponda wanachama wenzake walioshindwa kwenye kura za maoni kwa sababu mgombea anayefanya hivyo anaweza kuwa sumu kwa chama baadaye.

Lakini katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu uliofanyika Oktoba 28, hali ilikuwa tofauti katika jimbo la Kyela. Mgombea aliyependekezwa na chama kuwania ubunge katika jimbo hilo, Ally Mlagila maarufu Kinanasi, ambaye mbali na kutamba kuwa ni Mwenyekiti pekee wa CCM wa Wilaya aliyeruhusiwa kugombea ubunge, aliendesha kampeni ya nguvu kumponda mtangulizi wake, Dk. Harrison Mwakyembe, akidai kuwa hakufanya kitu chochote cha maendeleo kwenye jimbo hilo.

Mgombea wa CHADEMA baada ya kusoma upepo wa kisiasa katika jimbo hilo, alitumia nafasi hiyo kujinadi kwa kusifia miradi iliyofanywa na Dk. Mwakyembe, hatua ambayo ilionekana wazi kuanza kuungwa mkono na wananchi hususan wale ambao walikuwa hawapendezwi na kauli za kejeli zilizokuwa zinatolewa na Kinanasi.

Kilichonisukuma niandike uchambuzi huu ni kwamba hata baada ya uchaguzi kumalizika na Kinanasi kuibuka Mbunge wa Kyela, badala ya kuhangaikia maendeleo ya jimbo lake, ameendeleza kampeni dhidi ya mtangulizi wake na wote waliokuwa wanamuunga mkono. Kinanasi hivi sasa anatamba kuwa ni yeye na Magufuli tu ambao wana kofia mbili nchini hivyo ole wao ving'ang'anizi wanaomtetea Mwakyembe. Kwa kuwa nimeishi Mkoa wa Mbeya na Kyela, bado Mwakyembe ana ushawishi mkubwa kwa wapigakura (tofauti na wajumbe) na chama kinamhitaji leo na kesho.

Sina ushahidi kama kuna kiongozi yeyote wa ngazi ya mkoa au taifa ambaye ameibuka na kumkemea Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kyela kwa jinsi anavyokiendesha chama kibabe hivi sasa. Kibaya zaidi ni imani inayojengeka Kyela kuwa anayoyafanya yamebarikiwa "huko juu" japo mimi sitaki kuamini hivyo.

Mfano wiki iliyopita kulifanyika vikao viwili muhimu vya chama, kikao cha Kamati ya Siasa ya Wilaya na Halmashauri Kuu ya Wilaya ambavyo agenda kuu ilikuwa kufanya tathimini ya uchaguzi mkuu.

Vikao hivyo badala ya kujikita kwenye agenda vikaishia kumjadili Dk. Mwakyembe na wale ambao wanaamini walikuwa wakimuunga mkono. Kinachotafutwa hapo ni kutaka kuwashughulikia na pengine wafukuzwe katika chama, hatua ambayo haitakuwa na tija kwa CCM kwani Kinanasi bado ni mchanga sana kwenye CCM!

Taarifa kutoka ndani ya kikao cha Kamati ya Siasa ya Wilaya ni kwamba hoja hiyo ilikwama kwa wajumbe walio wengi kusisitiza kuwa Dk. Mwakyembe alishiriki vizuri kwenye kampeni kukisaidia chama.

Baada ya hoja hiyo kukwama, imeelezwa kuwa suala hilo lilifikishwa kibabe katika kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya na mbunge huyo ambaye vilevile ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya pamoja na wapambe wake, walitaka Mwakyembe aazimiwe kwa kushindwa kuifanyia kampeni CCM kata kwa kata.

Hata hivyo, wapambe hao, walitaka Dk. Mwakyembe aadhibiwe licha ya kwamba ni wao wenyewe wanaotajwa kumzuia kufanya kampeni kwenye kata kwa madai kuwa angeliwaharibia kura.

Kimsingi, kwa muda mrefu kumekuwa na mvutano ambapo wanachama wengi wa CCM wanamtaka Mlagila aache sasa porojo za kisiasa zinazoelekea kukigawa chama badala yake ahangaikie changamoto za maendeleo za wananchi.

Baadhi ya wanachama wa CCM wanaulaumu uongozi wa juu wa chama chao kwa kuwa na ndimi mbili kuhusu Kyela kutokana na kumruhusu Mwenyekiti wa CCM Wilaya kugombea ubunge kinyume cha kanuni na taratibu za chama.

Ikumbukwe kwamba Mbunge na Mwenyekiti huyo alishawahi kumsimamisha Dk. Mwakyembe na baadhi ya viongozi wa CCM , wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya, uamuzi ambao ulitenguliwa na vyombo vya juu vya CCM.

Akihutubia mkutano huo wa Halmashauri Kuu, mwenyekiti huyo alielekeza mashambulizi yake kwa baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya kwa kuendelea kumtetea Dk. Mwakyembe na kuahidi kuwa atawashughulikia.

Kutokana na minyukano ya kisiasa isiyoisha wilayani Kyela ambayo wengi wanaamini inachochewa na majeruhi wa Richmond, Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan Septemba 21, mwaka huu, akiwa kwenye kampeni wilayani humo, aliwaonya viongozi na wanachama wa CCM kuacha vidomodomo vya ufitini.

**Mungu ibariki Kyela, Mungu ibariki Tanzania**

## DARASA LA NDOA

# Uongozi wa familia wenye mafanikio



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka
0744000066

MPANGO asilia wa Mungu ni kwamba mume na mke waishi pamoja katika amani na utulivu. Mume na mke wanategemeana. Mungu aliumba mwanamume na mwanamke ili wahitajiane na kutegemeana katika maisha.

Pamoja na kwamba wajibu na majukumu yao hutofautiana, wana umuhimu sawa katika familia na jamii.Wote ni muhimu katika ustawi wa familia na jamii bora.

Maadiko matakatifu ya Mungu yanaonyesha na kuainisha nafasi na wajibu wa mume na mke katika familia. Jukumu kubwa alilopewa mwanamume ni kuwa kiongozi wa familia yake.

Katika kutekeleza jukumu la uongozi, mume amepewa mamlaka na Mungu ya kuongoza familia yake kwa upendo na si kiimla. Uongozi wa kiimla ndani ya familia nyingi umeharibu familia na watoto. Umeondoa mvuto wa baba kwa familia yake. Uongozi wa kiimla katika familia huua pendo la mke na watoto.

Mahali pengi uongozi wa namna hiyo umemfanya mke ajisikie ni mtu duni asiye na thamani na mchango katika familia. Wanawake wengi wamepoteza hali yao ya kujiamini kama mke na mama wa familia.

Pamoja kwamba baba ni kiongozi wa familia, hana budi kufahamu kuwa mafanikio katika kutekeleza majukumu yake ya uongozi katika familia yanategemea mke aliyenaye. Kwa hiyo, kujua kuishi na wake zetu kwa akili ni jambo la busara.

Ili mume aongoze familia yake kwa mafanikio, anahitaji kumfahamu mke wake na kutambua umuhimu wa uwapo wake katika familia. Wanandoa wanahitaji umoja na mikakati ya pamoja ili kukabili changamoto na kufanikiwa katika maisha yao.

Njia nzuri ya kushinda vita na maadui ni wanandoa kuishi kama timu moja yenye lengo na mwelekeo mmoja. Siku zote timu yoyote ina lengo la kushinda. Na familia kama ilivyo timu haina budi kuwa na malengo tene shirikishi ya kufikia kilele cha mafanikio.

**KANUNI 8 ZA UONGOZI WA FAMILIA WENYE MAFANIKIO**

Katika kufikia kusudi lolote lile kwenye maisha, mtu au jamii hawana budi kuwa na kanuni, miongozo na njia za kufuata ili kufikia mafanikio. Kadhalika, hata familia inapaswa kuwa na kanuni. Kwa kiongozi wa familia yenye mafanikio, kanuni zifuatazo ni muhimu;-

Mume amfahamu mke wake

Mume amfahamu mke wake anachokipenda na asichokipenda. Afahamu mahitaji yake ya msingi na kujitahidi kuyatimiza kadiri ya uwezo na hali inavyoruhusu. Mume afahamu uzuri na upungufu ya mke wake. Katika hilo pia, Mume amsaidie mke wake katika upungufu na kuonyesha upendo. Wanawake wana hitaji kubwa la kupendwa na mahaba (love and affection). Njaa ya mwanamke yeyote ni kupendwa. Wanaume wengi hawajui hitaji hili la wanawake.

Waume wasiwe wakatili kwa wake zao kwani ukatili huondoa hisia za mke kwa mumewe. Mwanamke anapoonyeshwa upendo, huridhika na maisha ya ndoa na hujisikia yeye ni mtu wa thamani na wa pekee. Kadiri mwanamke anavyopendwa, hali hiyo humwongezea hisia za mapenzi, huvutiwa na mume wake na kutoa ushirikiano mzuri.

Kwa asili, wanawake hupendwa kuguswa vizuri, kutomaswa tomaswa, kukumbatiwa, kuambiwa maneno mazuri, kupongezwa na kutambulika. Maneno yenye kuonyesha upendo, ni ya maana sana kwa wanawake. Pamoja na hayo, wanawake wanapenda ukaribu wa waume zao, hivyo wababa watengeneze mazingira ya kuwa karibu na wake zao. Ukiona mke hapendi ukaribu wa mume wake, basi ujue kuna tatizo la msingi linalohitaji kushughulikiwa.

Zaidi sana, wanawake wanapenda mwanaume mwenye kujua majukumu yake. Ni muhimu wanaume wafahamu kuwa, kinachowafanya waitwe wanaume ni majukumu waliyo nayo katika familia. Kwa hiyo, kutunza familia huongeza heshima na thamani ya uwepo wa baba katika familia yake.

**USHIRIKISHWAJI**

Wanawake wanapenda sana kushirikishwa hasa wale wenye umri kati ya miaka 40 hadi 50. Uongozi shirikishi katika familia una baraka nyingi kuliko uongozi wenye misingi ya ubinafsi.

Ushirikishwaji unapokosekana huzaa migogoro ndani ya familia. Wanaume wanaotambua nafasi za wake zao katika familia huwashirikisha katika uamuzi na usimamizi wa familia. Hata hivyo, mke akiona hashirikishwi inabidi ajitathmini na kumuuliza mume wake ili kujua sababu za kutokushirikishwa kwani inawezekana wakati mwingine tatizo liko kwa mwanamke mwenyewe. Mwanamke akijua tatizo ni vyema ajisahihishe ili ashirikishwe.

Wanawake wanaposhirikishwa wanajisikia kutambulika, wanajiamini na kufanya vizuri zaidi. Wanaume wanaowashirikisha wake zao, hufanikiwa sana. Mume amtambue mke wake kuwa ni mwenzake mwenye mchango katika masuala ya familia na mwenye haki ya kushirikishwa. Mwanamke husikia fahari anaposhirikishwa mambo yanayohusu mustakabali wa familia yake.

**MAWASILIANO BORA**

Mawasiliano katika ndoa ni daraja muhimu linalounganisha ndoa. Ni injini inayofanya ndoa iwe katika mwendo. Kumjua mwenzi kunaanzia na mawasiliano. Mume na mke wanapokuwa hawana mawasiliano mazuri baina yao, wanakosa kufahamiana vizuri, uhai katika uhusiano huondoka hivyo hudumaza pendo la ndoa. Mawasiliano mazuri yanapokuwapo heshima na thamani ya uhusiano huongezeka.


**Itaendelea Jumapili ijayo**

• **Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care (TaMCare) Foundation inayojihusisha na Masuala ya Malezi ya Watoto. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa baruapepe: info@tamcare.or.tz**

MAISHA
Desemba 20, 2020
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 12



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Jinsi ya kung'arisha dirisha

## Vitumbua vya Nazi

Ukurasa 14



# Unadhifu wa mwanamke akiwa ofisini



Ukurasa 14

# Katika umri huu mtoto hujua zuri, baya

**Na Moses Ismail**

Ni kawaida kwamba katika umri wa kuanza kutambaa hadi miaka miaka mitano, tunawachukulia watoto wetu kuwa hawajui zuri wala baya katika matendo yao wanayofanya.

Tunawaita jina zuri tu la'malaika' tukimaanisha hawajui lolote na hawawajibiki sana katika yale wanayoyafanya tukiamini hulifanya bila kujua uzuri au ubaya wake.

Kwa sababu hiyo, watoto wa umri huo hatu waonyi kwa 'ukali sana' kwa yale anayoyafanya, tunawachukulia poa tu tukisema; "ni ututo tu, akikua ataacha".

Bahati mbaya wapo wanaokua na tabia zao za utoto ambao hawakataziki tena pale wanapofanya ukorofi katika umri usiopaswa kufanya tena ukorofi. Wanakuwa manunda!

Idadi ya watoto hao, manunda, ni kubwa na hiyo inasababisha malalamiko ya kuwapo kwa watoto watukutu katika jamii.

Hili linajenga swali la msingi, kwamba umri hasa wa kumfundisha mtoto tabia njema kwa kumfundisha kuwajibika kwa tabia zake ni upi?

Kwa elimu ya tabia ya asili ya mwanadamu, inaonyesha kwamba mtoto huanza kupokea mafunzo ya mema na mabaya tangu akianza kutambaa tu na hujifunza 'kuwajibika' kwa kufuatilia makatazo ya wakubwa zake kwa kila analolifanya.

Kwa mfano, chukulia mtoto huyo anayetambaa, katika kutambaa kwake anaelekea kwenye sufuria iliyowekwa maji, lakini kabla hajaifikia sufuria hiyo anageuka na kukutazama wewe mzazi wake usoni.

Mnapokutanisha macho yenu, anakuangalia kwa makini na kusoma kinachoongelewa na uso wako, anapogundua kuwa hutaki aendelee kutambaa kusogelea sufuria hiyo anaamua kujichekesha na kufanya jambo jingine kabisa tofauti na kuifuatilia sufuria hiyo.

Na iwapo kama utakuwa makini na tendo hili la mwanaoa asiyezidi miezi tisa utagundua kuwa kwa kila jambo analotaka kufanya, katika mazingira ya karibu yako, basi ni lazima ageuke na kuangalia uso wake kabla ya kuamua kufanya ama kuacha.

Unaweza kuonyesha dalili zote za kumkataza asisogelee sufuria hiyo, kwa kumtazama tu, lakini akajaribu kulifuata ili apata uhakika kama uso na macho yako yanamaanisha kweli anachokiona?

Katika hali hiyo, mzazi utatoa sauti ya 'acha' au 'rudi hapa', pia atakuwa makini kuliko wewe kwa kusikiliza sauti hiyo, akiona ina upole na haina msisitizo au taharuki, basi atajichekesha na kuendelea na mambo yake.

Hii ndiyo saikolojia ya watoto 'wachanga' wanapoanza kujifunza ni lipi zuri la kufanya na nilipi baya analotakiwa asilifanye.

Ni hatua muhimu sana katika kumjenga mtoto kitabia.

Unapomjengea mtoto misingi ya kujua la kufanya au la kuacha katika umri huu, unamfanya awe mwepesi wa kusikiliza na kuwa na adabu na wala haihitaji kiboko ili kumfanya atii kile anachotakiwa au asichotakiwa kufanya na hili uganda katika ubongo wake hadi ukubwani.

Kwa kumtengeneza mwanao akiwa katika umri huo wa kutambaa kwake, miezi saba au tisa ya mwanzo ya maisha yake, ni jambo muhimu na linalopaswa kufanywa na kila mzazi kwa mustakabali wa kuwa na tabia nzuri na mwenye kusikia.

Usichukuli kabisa kwamba kile anachokifanya mwanao huku akiwa anakutizama usoni kama ni kitu cha kitoto, hapana. Anapokuangalia usoni ni kwamba anajaribu tu kujiridhisha kwa akili yake ya tabia za maumbile kama anachofanya ni sawa au si sawa.

## QUIZ

**NA HAMIS KIDAGO**
0657 207168

### LE QUIZ DU WEEK


Le Verbe Suivre – Kitenzi "Fuata"

1. Kamilisha unyumbuaji wa kitenzi "Fuata" katika nyakati mbalimbali kama zilivyoainishwa hapo chini.

Indicatif
present
je ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………
imparfait
je ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………
futur simple
je ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………
passé simple
je ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………
passé compose
j' ai ……………
tu as ……………
il/elle a ……………
nous avons ……………
vous avez ……………
ils/elles ont ……………
plus – que – parfait
j' avais ……………
tu avais ……………
il/elle avait ……………
nous avions ……………
vous aviez ……………
ils/elles avaient ……………
futur anterieur
j' aurai ……………
tu auras ……………
il/elle aura ……………
nous aurons ……………
vous aurez ……………
ils/elles auront ……………
passé anterieur
j' eus ……………
tu eus ……………
il/elle eut ……………
nous eumes ……………
vous eutes ……………
ils/elles eurent ……………
Conditionnel
present
je ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………
passé
j' aurais ……………
tu aurais ……………
il/elle aurait ……………
nous aurions ……………
vous auriez ……………
ils/elles auraient ……………
Infinitif
present
……………
passé
……………
Participe
present
……………
passé
……………/……………
……………/……………
……………
Imperatif
present
……………
……………
……………
passé
……………
ayons ……………
……………
Subjonctif
present
que je ……………
que tu ……………
qu' il/elle ……………
que nous ……………
que vous ……………
qu' ils/elles ……………


## WATOTO

### PAKA RANGI




### CHEKA KIDOGO

**Mazungumzo kati ya marafiki wawili yalikua kama ifuatavyo;**
**Juma: Habari yako kijana?**
**John: Safi tu nambie,**
**Juma: Aiseee! muda kweli naona unahangaika na bodaboda tatizo nini kwani?,**
**John: Dah! Namsaidia huyu kijana Raymond kutafuta kiki za haraka aonenekane kwenye gazeti eti.**
**Juma: Ooohhhh!! Kweli huyu mzima!**



**Hifadhi ya Gombe inapatikana mkoa gani?**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Wengi wanateswa kwa maneno yaliyotamkwa

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Tumekuwa tunajadili vyanzo vya matatizo yanayotutesa hivi leo kumbe mengine yalianzia huko tulikotoka enzi za mababu na mabibi zetu.

Mfano mzuri nilioukazia sana ni roho ya mitala, yaani ndoa za wake wengi. Kama bibi au mama aliolewa akaachika, kisha akaolewa tena, uwezekano ni mkubwa mabinti au wajukuu zao wakarithi hiyo roho.

Msomaji wetu mmoja akasema; "Mimi yalinikuta nilioa mke ambaye kwao hawaishi kwa mume. Huyu wangu alishaolewa mara mbili na kote huko alizaa watoto wawili kwa kila mwanamume.

"Mimi nina watoto wane naye akanikimbia akaenda kupanga nyumba. Baadaye akanifuata eti tuendelee kuwa wapenzi akae kwake nami nikae kwangu ila tuwe tunaonana. Naomba ushauri. Naitwa Douglas",

Hivyo ndivyo anavyomaliza ujumbe wake.

Ukichimbua historia ya mwanamke huyu upande wa wazazi wake, utagundua kwamba ni tatizo ambalo linawapata wengi wa wanafamilia hiyo tokea enze za mababu. Ni mnyororo ambao bila kukatwa kwa maombi utaendelea kuteza kizazi hata kizazi.

Ni mambo mengi sana yamewakumba vijana wasijue cha kufanya. Kumbe kipo chanzo cha matatizo yanayowasibu leo. Hebu kwanza hapa niweke ujumbe wa baadhi yao kwa yale wanayopitia."Mimi naomba msaada. Yaani mimi sijui nina tatizo gani. Hakuna mwanamke ninayetaka awe mpenzi wangu ananikubali, hayupo. Naumia sana na sijui la kufanya. Kila mwanamke ananikataa, wengine hata nikiwaita tu, nakutana na tusi. Nifanyeje? Niko Mbeya.

Mpenzi msomaji, unaona jinsi watu wanataabika katika maeneo mbalimbali ya maisha yao. Hata hivyo, bado tunarudi pale pale kwamba hakuna tatizo lisilo na chanzo. Kijana anayehangaika katika uhusiano, kila anayemsogelea ama hamtaki au anamtukana.

Hapa ameghubikwa pia na roho ya kukataliwa. Pia roho ya ushirikina au nguvu ya maneno. Pengine katika familia upo ushirikina. Yawezekana miongoni mwa wanafamilia ni mshirikina anayemtesa kijana huyu.

Wapo watu wanaoonea wivu watoto wa wenzao pengine wanasomeshwa vizuri, wana akili shuleni lakini wale watoto wao hawana neema hiyo. Kwa mantiki hiyo huweza kutumia kila mbinu, ikiwamo ya ushirikina kuhakikisha kuwa wanaharibu hatma za wale wanaosoma shule nzuri.

Wengine hudiriki hata kutumia maneno kulaani watoto wa wenzao. Inawezekana ni wivu tu hata mtu kufikia hatua ya kurushiana maneno na jirani yake. Mfano, "tuone kama mwanao atamaliza shule, watoto wako hawatafika chuo kikuu" na kadhalika.

Maneno yanapotamkwa lazima mwishoni yatakuwa ni kizuizi kibaya sana. Hii ni kutokana na ukweli kwamba maneno ni roho. Hii inamaanisha kwamba maneno ni nguvu. Maneno yana uwezo wa kumtia mtu nguvu ya kuendelea kwenye kufanikiwa au kumrudisha nyuma.

Kabla mtu hajafungua mdomo wake na kuongea, yampasa kutafakari kwanza na kujiuliza; Je, maneno yangu yanatia moyo, yanakwanza watu, yanaua watu kiimani, yanatia hofu, yanavunja watu moyo, yanajenga au nayabomoa?

Yamkini yapo maneno yaliyotamkwa na wazee wetu zamani ambayo yanaishi hata leo, kwani kama nilivyosema hapo juu kuwa maneno ni roho. Maneno yanafuatilia kizazi hata kizazi. Kama yapo maneno yaliyoitamkwa au maagano yaliyowekwa na wazee wetu enzi hizo kwamba katika ukoo wetu hatatoka daktari, hakika itakuwa kama ilivyotamkwa.

Kama ilitamkwa familia fulani hawatafikia elimu ya chuo kikuu, itakuwa hivyo hivyo. Maneno hayafi hadi yafutwe. Utaona familia nyingi wanafikia darasa la saba hawaendi zaidi ya hapo. Wengine wanaishia sekondari, wengine hadi chuo kikuu lakini wanapotafuta kazi hawapati. Wengine hadi wanazeeka hawaoi wala hawaolewi.

Hebu msikie mpendwa huyu katika ujumbe wake aliotuma wiki hii. Anasema hivi,"Dada Flora, mimi naitwa kaka Paty wa Bagamoyo, nimesoma kwenye NIPASHE Maisha Ndivyo Yalivyo. Ni kweli mnyoroo ni mbaya sana. Mimi nina umri wa miaka 38 sijaoa wala sina mtoto. Mjomba wangu ana miaka siyo chini ya miaka 50 hajawahi kuoa wala hana mtoto. Hii ni nini?

**Msomaji wangu, Lazima watu watafute sana nguvu ya Mungu kufuta hayo maneno. Mungu ni mwaminifu, huchunguza mioyo, tukiomba kwa dhati laana za aina hiyo hufutika.**

**Tuishie hapa hadi wiki ijayo. Ukiwa na kisa, maoni, ushauri nitumie ujumbe kupitia 0715268581. Namba hii pia ipo WhatsAPP.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Bei ya saruji, nondo sasa maumivu

BEI ya saruji bado haijashuka kama ilivyoelekezwa huku sababu kubwa, ikiwa ni kuadimika kwa kuwa bado viwanda havijazalisha kwa kiwango kinachotakiwa.

Hali hii ni maumivu makubwa kwa wajasiriamali wa biashara ya matofali ambao wanashindwa kuzalisha kwa wingi na wanalazimika kupandisha bei ili kufidia gharama zingine zilizosababishwa na bidhaa hiyo.

Wakati hali ikiwa hivyo bei ya nondo imeanza kupaa kutoka Sh. 19,500 hadi 20,500 huku tani moja ikipanda kutoka Sh. milioni 1.6 hadi milioni 1.9 jambo ambalo ni maumivu makali kwa watu wa kawaida ambao wanapambana kujenga makazi yao.

Kupanda kwa bei hizi kuna madhara makubwa kiuchumi kwa kuwa athari yake inakwenda moja kwa moja hadi kwa mtu wa kawaida ambaye mkate wake wa siku unategemea shughuli za siku.

Kama watu watasitisha ujenzi wa nyumba wakisubiri kushuka bei ya bidhaa hizo maana yake walioajiriwa katika vijiwe vya kufyatua matofali ambao hulipwa kwa idadi ya matofali waliyofyatua watasimama kufanya kazi. Wauza mchanga na kokoto nao watasimama maana yake hawatapata kipato cha siku.

Pia kuna mafundi ujenzi ambao hawataendelea na kazi kwa sababu watakosa kipato cha familia zao. Lakini pia kuna vibarua wengine ambao katika ujenzi hujipatia chochote kwa ajili ya maisha yao wote hao atakuwa nyumbani hawana fedha.

Aidha, maduka yanayouza bidhaa za nondo na ujenzi kwa ujumla yatapungukiwa wateja kwani katika kukabiliana nahali ngumu watalazimika kupunguza wafanyakazi, ambao nao watakwenda kuungana na waliokosa cha kufanya na kukaa nyumbani bila kipato.

Kama baba na mama kazi zao ni katika sekta ya ujenzi na wamepunguzwa, hali ya maisha yao itakuwa ngumu kiasi cha kuwafanya kushindwa kumudu mahitaji ya msingi ya familia, baadhi wanaweza kushawishika kufanya mambo yasiyofaa katika jamii.

Kama haitoshi mtu huyu bado atashindwa kupika ka mafuta kwa kuwa nayo yampanda bei, maana yake itamlazimu kuchemsha chuku chuku ili siku ipite na mwishowe mwili utakosa mafuta na kuingia maradha, na mtu huyu ambayee hana fedha ya kwenda hospitali kwa kuwa hana bima basi huenda ikawa ndiyo mwisho wa maisha yake.

Ni muhimu sana suala la kupanda kwa bidhaa hizi kukaangaliwa kwa jicho la mnyororo wa athari zinazowakumba wengi ambao maisha yao ya kila siku yanatarajia kutoka kwenye sekta ya ujezi.

Viongozi wa kitaifa walitangaza hatua mbalimbali lakini bado bidhaa hiyo imesimama kwenye bei ya awali ambayo kwa Dar es Salaam ni Sh. 17,000 hadi 17,500, jambo ambalo ni maumivu.

Ni vyema kushughulikia mzizi wa tatizo kwa kuwa ndio utakuwa tiba sahihi kwa tatizo hilo. Si rahisi kwa wauzaji kupandisha bei ikiwa bidhaa hiyo inapatikana kwa wingi, wengi wanaleza kuwa haipatikani na wanalipia bidhaa hiyo viwandani wanakaa hadi mwezi mmoja ili kupata.

Kukosekana kwake ndiyo sababu kubwa, hivyo la kushughulikiwa ni kwani inaadimika katika maeneo mbalimbali nchini wakati kasi ya uzalishaji kwenye viwanda ikiwa ni ile ile, ni vyema mzizi wa tatizo ukajulikana na kushughulikiwa.

Hali ikiachwa ilivyo, mnyororo wa manufaa utaumiza wengi kwa kuwa wapo wengi katika sekta hiyo inawapa kipato cha kupata mahitaji ya msingi kama nguo, chakula na malazi.

Tunakwenda Januari ambayo wazazi wanatakiwa kuwajibika kulipa ada na kununua mahitaji ya msingi ya watoto wao. Kama hawatakuwa na fedha , hata namna ya watoto kusoma itakuwa taabu kwa kuwa wapo watakaoshindwa kutokana na kukosa chakula na kama una njaa ni wazi kuwa mwanafunzi hawezi kuelewa kinachofundishwa darasani.


Ni muhimu athari zikaangaliwa kwa kina na isiwe kwa wajenzi pekee bali kwa watu wa kawaida ambao sekta hiyo inawategemea kwa ajili ya maisha ya kila siku.

**Tutafakari!**



# HAJI MANARA

Picha ambazo hujawahi kuziona kuhusu harusi ya Msemaji wa Timu ya Simba, Haji Manara.







# MITINDO



# KUWA MAKINI
# MAVAZI YA 'MODO' YANA RAHA, LAKINI YANA KARAHA

UMAKINI siku hizi nguo za kubana mwili maarufu kama 'Modo' zimepata umaarufu na kupendwa na kila rika hasa vijana.

Ni jambo la kawaida kukutana na watu walipigilia suruali, shati, fulana au suti zikiwa katika mtindo wa kubana mwili.

Uvaaji wa nguo za aina hii unaonekna ni wa kisasa zaidi, hivyo kila mtu anataka kuonekana anakwenda na wakati katika suala zima la uvaaji.

Wachambuzi wa mavazi wanasema mitindo ya nguo ya kubana siyo mipya duniani, ilikuwa inatumiwa zamani lakini kwa sasa imeboreshwa kwa kuongezewa vikorombwezo mbalimbali inayovutia.

Hata hivyo, aina haya ya mavazi yana athari kwa watumiaji endapo watatumia muda mrefu.

**Nguvu za kiume**

Wataalamu wanasema endapo mtu akipenda kuvaa suruali ya kubana kila wakati, kuna hatari ya kupungukiwa na nguvu za kiume kutokana na mishipa ya fahamu kubanwa na kukosa nguvu ya mawasiliano.

**Mwili kukosa uwezo wa kutoa uchafu**

Kwa kawaida mwili unatoa uchafu kwa kusaidiwa na vitundu kwenye ngozi, hivyo inapobanwa kazi hiyo haifanyika taratibu na kusababisha mishipa ya damu kujaa mafuta.

Unashauriwa nguo za aina hiyo kuvaa kwa muda fulani na kasha kutumia nguo inayoacha wazi mwili.

**Saratani ya ngozi.**

Kurundikana kwa uchafu katika vitundu vilivyopo kwenye ngozi inasababisha seli zilizoharika kutopata nafasi ya kutoka nje, hivyo kuna hatari ya kugeuka kuwa saratani.

Ni muhimu kila unapotumia nguo za kubana kwa muda mrefu kufanyiwa massage ya mwili wote ili kuondoa uchafu.

## UREMBO



# Unadhifu wa mwanamke akiwa ofisini

NI jambo zuri kwa mwanamke kuwa nadhifu wakati wote, iwe nyumbani, kazini au sehemu nyingine.

Kwa mwanamke jambo la kujiweka nadhifu wakati wote ni muhimu sana, haijalishi unapitia katika hali gani.

Ni vema kukumbuka kwamba unapojiweka nadhifu hata kama una matatizo si rahisi mtu mwingine kufahamu.

Wanawake ndio taswira sahihi ya kila ofisi, wanapokuwa nashifu kuanzia mwili hadi mavazi kila mtu anapoingia anakuwa na imani ya kupata huduma bora.

Jambo la muhimu unapokwenda ofisini ni lazima kuhakikisha mwili wako upo safi na unaovutia.

Unashauriwa sura na maungo yaonyeshe yana furaha wakati wote ikiwemo tabasamu pana.

Pia pangilia vyema nguo zako, pamoja na kuzinyoosha vizuri.

Unashauriwa kuwa kila siku kuwa na nguo za aina na rangi tofauti, viatu vinavyokupa uhuru wa kufanya kazi na manukato yenye harufu nzuri.

Mwanamke anayejipenda hawezi kuwa na ujasiri au kujiamini kama akiwa mchafu.

Kuwa nadhifu hakuhitaji gharama yoyote, ni wewe tu kuamua na kujituma katika hilo.

## MAPISHI

Na Mary Geofrey



# VITUMBUA VYA NAZI

VITUMBUA vilivyowekwa nazi na kiungo cha hiliki vinapendwa na watu wengi kutokana na ladha yake nzuri.

Mara nyingi tumezoea kupika vitumbua vya kawaida lakini leo tutaelezana namna nzuri ya kupika vitumbua vya nazi na iliki.

**Maandalizi**

Vikombe 2 mchele, vijiko vya chai kimoja na nusu

kikombe kmoja na nusu cha la nazi, kijiko cha chai nusu cha chumvi na nusu kikombe cha sukari.

Pia weka kijiko kimoja cha hiliki iliyosagwa, nusu kikombe cha mafuta ya kupikia. Osha na loweka mchele usiku kucha.

Chuja maji, weka pembeni, chemsha tui la nazi kwa sekunde 30 au mpaka liwe ya uvuguvugu kiasi katika moto wa wastani.

**Namna ya kupika**

Chukua mashine ya kusagia, weka mchele, tui la nazi, iliki, sukari, chumvi na hamira na saga mpaka ilainike vizuri.

Kama mashine yako ni ndogo, weka kidogo kidogo mpaka umalize mchanganyiko wote na mimina mchanganyiko kwenye bakuli, funika bakuli, acha mchanganyiko uumuke kwa lisaa moja au mpaka ujazo uzidi mara mbili yake.

Weka mafuta kwenye kila shimo la chuma cha vitumbua, mwagia mchanganyiko kwa ujazo robo tatu ya kila shimo.

Acha vitumbua vianze kuiva kwa dakika mbili hadi tatu au mpaka vianze kuwa na rangi ya kahawia na kona zianze kukauka kiasi.

Kwa kutumia kijiti cha mishikaki, geuza kitumbua upande wa pili, acha viive kwa dakika nyingine 3, au mpaka viwe na rangi ya kahawia

Ipua vitumbua, weka kwenye bakuli lenye tissues za jikoni ila mafuta yachuje. Vinaweza kuliwa vya moto au vya baridi.

# MAISHA NI NYUMBA

## Na Elizabeth Zaya

# JINSI YA KUNG'ARISHA DIRISHA



DIRISHA la kioo ni moja ya vitu vinavyochangia kung`arisha nyumba.

Ili dirisha liendelee kuwa bora na kung`arisha nyumba lazima lisafishwe.

Usipoweka kipaumbele katika jambo hilo usishangae kuona mvuto wa nyumba yako ukaanza kufifia kidogokidogo na mwisho wake ukaichukia nyumba kabisa.

Usafishaji wa dirisha ni lazima uwe na muda maalum ambao hakuna jua kali.

Kwa sababu unaposafisha wakati wa jua kali, maji unayomiminia katika dirisha lako hukaushwa kabla ya kupitisha sponji na hivyo kukuchukulia muda mwingi na pia haliwezi kung`aa vizuri na huacha ukungu.

Wakati unasafisha unatakiwa uwe pia na dawa maalum au kama unatumia maji si vibaya ukadondoshea kidogo vitone hata viwili vya maji spesho yenye mchanganyiko wa limao, maarufu kama 'vinegar'.

Baada ya hapo unalowanisha 'sponji' yako ama kitambaa laini kwa kuchovya kwenye maji hayo na kuanza kusafisha katika dirisha lako.

Hakikisha unasafisha kuanzia juu kushuka chini, ili uchafu wote utiririkie kwenda chini na kukuhakikishia kuwa hakuna uchafu utakadondokea kwenye sehemu ambayo imeshasafishwa tayari.

Kama eneo la dirisha unalotaka kusafisha ni chafu sana ama kuna vumbi jingi au utando wa buibui, futa kwanza kwa kitambaa kikavu kabla ya kusafisha na maji.

Uwe makini kuchunguza uchafu uliopo kwenye kona za madirisha yako.

Epuka kuweka maji mengi kwenye sponji ama kitambaa unachotumia kusafishia ili yasimiminikie chini sehemu ambayo siyo ya dirisha iwe ukutani ama sehemu nyingine isiyohusika.

Hakikisha unasuuza na kukausha dirisha lako kwa kutumia kitambaa kikavu na laini na baada ya hapo rudia tena kwa ajili ya kuling`arisha.

Kama utakuwa na dawa maalum ya kusafishia itapendeza zaidi kuipulizia kidogo katika dirisha huku ukifuta kwa kutumia kitambaa cha pamba ambacho hakitoi nyuzi.

Hakikisha dawa unayotumia kusafishia ni ile ambayo haiwezi kuharibu ama kupausha mbao za dirisha lako.

Kama dirisha lako ni la kioo, hakikisha sponji ama kitaamba ulichotumia kusafishia kioo ni tofauti na kile unachosafishia kwenye flemu ama kona za dirisha lako.

Katika maeneo ya flemu na kona, safisha kwa kutumia kitambaa kigumu zaidi ambacho kitabeba uchafu wote kwa sababu eneo hilo huhifadhi uchafu mwingi.



# MPANGILIO

# DONDOO MUHIMU KWA AJILI YA KUONGEZA MWANGA CHUMBANI WAKATI WA MCHANA


Wakati wa kutundika pazia hakikisha unatumia fimbo sahihi.

Hii ina maana kuwa fimbo za pazia ziwe laini za kuteleza kwa kuruhusu pazia kufunguka kwa urahisi.


Maeneo kama sebuleni paka rangi nyepesi inayoakisi mwanga, na hata kama unapendelea rangi nzito basi waweza kuziweka kwenye maeneo mengine.

Sawambaza mwanga unaoingia kwa kutukia kioo kikubwa kwa kurudisha chumbani mwanga kidogo unaopatikana.

Weka pazia nyepsesi lakini zenye maua mengi madogodogo na yaliyo karibu karibu chumbani ili kuruhusu mwanga kupita.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
SHETANI GANI ALIYENIRUBUNI KAMA ALIVYO-RUBUNIWA "ADAM!"
KUJINUNULIA MIGARI YA KIFAHARI
NILIKUWA SIJUAGI KUMBE HATA SHOTI' KATI ZINAKUWA NDEFU KAMA UJAZOEA KUCHAPA 'RAPA'
ILE NDOTO YA JANA NACHARAZWA FIMBO NA MKE WANGU INAMAANA GANI?
NILILALA NA POMBE NIKAAMKA NA ALAMA MGONGONI
KRISMASI HII NAKWENDA KUHESABIWA LAKINI KURUDI TENA JIJI LA WATU LABDA USHUKE MUUJIZA
UWANAKIJIJI NAUONA!
UKATA
DAR
MKOA
NIMEMISS KUUZA SURA KWENYE TIVII... ILIKUWA HAIPITI SIKU BILA KUUZA... "WAJUMBE HATARI"
KIONGOZI NAKUONA HAPO UNAJIEPENDELEA
NA MIMI NAKUONA UNAVYONIKOLEA...
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...SIO UKIPATA, HATA UKIKOSA RINGA...

## Waasi Afrika ya Kati waungana

**BANGUI,** Jamhuri ya Afrika ya Kati

VIONGOZI wa waasi kutoka vikundi vitatu nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati, wametangaza kuunda muungano kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu.

Shirika la Habari la AFP limenukuu taarifa iliyotolewa jana na viongozi hao ambao vikundi vyao vinadhibiti eneo kubwa katika nchi hiyo dogo na masikini barani Afrika.

Hatua hiyo inaweza kuzidisha machafuko ambayo tayari yameongezeka kuelekea uchaguzi wa rais na wabunge utakaofanyika Disemba 27 mwaka huu.

Upinzani tayari umetangaza kususia uchaguzi huo kutokana na wasiwasi wa kuwapo udanganyifu na wizi wa kura.

Hayo yanajiri wakati Umoja wa Mataifa umetuma ujumbe wake wa kulinda amani nchini humo baada ya kuongezeka kwa mashambulizi ya waasi yanayolenga kuvuruga uchaguzi huo.

**DW**

## Marekani yaikemea Urusi kwa udukuzi

**WASHINGTON,** Marekani

WAZIRI wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani, Mike Pompeo, ameilaumu Urusi kwa shambulio kubwa la mtandao dhidi ya mashirika ya serikali ya nchi hiyo.

Akizungumza katika kipindi cha redio, Pompeo alisema Urusi ilifanya majaribio kadhaa ya kudukua mifumo ya kompyuta ya idara ya usalama wa taifa hilo.

Wataalamu wa usalama walisema shambulizi lililofanywa linaweza kuruhusu wadukuzi kufikia mifumo ya kompyuta bila mipaka pamoja na mifumo muhimu ya serikali na huduma nyengine.

Idara ya Usalama wa Taifa iliwataka watumiaji wa mitandao kuwa makini ili kuzuia kudukuliwa kwa data za kijeshi na nyenginezo.

Rais mteule Joe Biden, alielezea wasiwasi wake juu ya udukuzi huo, huku Seneta wa Republican, Mitt Romney, aliituhumu nchi ya Urusi kutumia fursa ya ukimya wa Marekani kuendesha uhalifu huo.

**DW.**



Askari wa Umoja wa Mataifa wa kulinda amani nchini Afrika ya Kati, akizungumza na watoto kama njia ya kuwa karibu na jamiii. Nchi hiyo itafanya uchaguzi wake mkuu Desemba 17 mwaka huu. **(PICHA: AFP)**

# Marekani yaidhinisha chanjo ya pili

**WASHINGTON,** Marekani

MAREKANI imeidhinisha chanjo ya pili ya corona ya Moderna ambayo itasambazwa na kupewa raia wake mapema mwakani.

Mamlaka ya Kusimamia Usalama wa Chakula na Dawa nchini humo, (FDA) iliidhinisha chanjo hiyo iliyotengenezwa Marekani karibu wiki moja iliyopita.

Chanjo ya kwanza kuidhinishwa ni ile ya Pfizer/BioNTech ambayo imeanza kutolewa kwa raia wake.

Taifa hilo limekubali kununua dozi milioni 200 ya chanjo ya Moderna, na milioni sita kati ya hizo huenda ziko tayari kusafirishwa.

Nchi hiyo ina idadi kubwa ya vifo vilivyotokana na ugonjwa wa corona, huku ikishuhudia viwango vya juu vya maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo.

Kamishena wa FDA, Stephen Hahn, alisema kuidhinishwa kwa dharura kwa chanjo hiyo siku ya Ijumaa kunaashiria kufikiwa kwa hatua nyingine muhimu katika juhudi za kukabiliana na janga hilo.

Hatua ya kuidhinishwa kwa chanjo hiyo ilifikiwa baada ya jopo la wataalamu kupiga kura siku ya Alhamisi, huku wito ukitolewa kwamba ubora wa chanjo ya Moderna unazidi madhara yake kwa watu waliyo na umri 18 na zaidi.

Wadhibiti waliripoti mapema wiki hii kwamba chanjo ya Moderna ilikuwa salama na inafanya kazi kwa asilimia 94.

Rais wa Marekani Donald Trump, aliandika katika mtandao wake wa Twitter saa kadhaa kabla ya kut\olewa tangazo rasmi, kuwa chanjo hiyo imeidhinishwa kwa kishindo na itaanza kusambazwa mara moja.

Rais mteule Joe Biden, ambaye anajiandaa kupewa chanjo siku ya Jumatatu, alisema kuidhinishwa kwa chanjo za sindano za Pfizer na Moderna inawahakikishia siku njema huko mbele. Hata hivyo, alionya vita dhidi ya Covid-19 havijaisha.

Kampuni ya Moderna inatarajia kuzalisha hadi dozi bilioni moja kiasi kinachoweza kutumiwa ulimwenguni kote ifikapo mwakani.

**BBC**

# Yemen waomba msaada kuokoa watoto mapacha

**SANAA,** Yemen

MADAKTARI wa Hospitali moja nchini Yemeni, wameomba msaada wa dharura wa kimataifa kuokoa maisha ya mapacha wawili waliozaliwa wakiwa wameungana.

Mkuu wa hospitali ya Al-Sabeen, iliyopo mji mkuu wa Sanaa, ambako watoto hao wa kiume walizaliwa alisema watoto hao wako katika hali hatari na wanahitaji upasuaji wa dharura..

Uwanja wa ndege wa Sanaa umefungwa kutokana na vita vya muda mrefu vinavyoendelea nchini humon na kusababisha kuharibu miundombinu na mfumo wa afya. Kituo cha misaada cha Saudi Arabia, kilicho na makao yake nchini humo, kilisema kinatathmini ikiwa itaweza kusaidia

"Uchunguzi wa kimatibabu umeonyesha kuwa mapacha hao wameungana lakini kila mmoja ana moyo wake, lakini sehemu ilipo na moyo wa mmoja wao sio wa hali ya kawaida," Mkurugenzi wa hospitali hiyo aliliambia shirika la habari la AFP .

Alisema hospitali hiyo haina vifaa muhimu vinavyohitajika ili kuokoa maisha ya mapacha hao kwa kutoa taswira kamili ya viungo gani vilivyoungana.

Ikijibu ombi hilo, Shirika la misaada la mfalme Salman, liliandika kupitia mtandao wa Twitter, "KSrelief itajitolea kusaidia watoto hao kuchunguzwa na wataalamu wa Saudi Arabia na kutathmini uwezekano wa kuwatenganisha,"

**BBC**

MAKALA

# Hujachelewa



Na Magabilo Masambu

**Ukweli ni kwamba tunapaswa kujifunza maisha kwa wengine lakini ni mwiko kuiga maisha hayo. Kila mtu ana siri ya mafanikio yake na wengi wanapoeleza juu ya mafanikio yao, huwa hawasemi ukweli na mara nyingi husema sehemu tu ya yale watu wanayoyaona juu yao.**

KATIKA kuzungumza mambo mbalimbali na baadhi ya watu wenye umri mkubwa, kuhusu maisha, nimegundua kwamba watu wengi wanapozeeka huwa wanajilaumu kwa mambo ambayo hawakuyafanya katika maisha na hawajutii kwa mambo ambayo waliyafanya ama kwa makosa au kwa kupatia.

Utasikia anasema ningekuwa kijana, ningefanya hivi na vile au ungekuwa wakati wangu ningefanya hili na lile. Ni kweli kwamba kuna umuhimu wa kufanya kila jambo kwa wakati, lakini swali je, ni wakati gani sahihi wa kufanya jambo lipi?

Kuna mambo katika maisha unaweza kuyafanya kwa wakati, lakini matokeo ya mambo hayo yakachelewa kutokea.

Mfano unaweza kuoa ili upate watoto mapema lakini ukapata watoto katika uzee wako. Katika maandiko kuna hadithi ya Sara na Abraham, katika umri wa miaka 99 ya Abraham na 89 ya Sara ndipo walipopata mtoto, baada ya kupewa taarifa na malaika kwamba: "Mwaka ujao wakati kama huu mtapata mtoto."

Desemba 8, mwaka huu, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mzee Samuel Mutasa, mwenye umri wa miaka 82, alitunukiwa Shahada ya Udaktari (PhD). Pengine wengi wetu tunaweza kushangaa imewezekanaje katika umri huu kwa mzee ambaye alistaafu kazi toka mwaka 1993 akiwa na umri wa miaka 55 leo baada ya miaka 37 anatunukiwa shahada hiyo? Tuna la kujifunza hapa.

Kutokuwa na ndoto yoyote ya kutimiza katika maisha, inaweza kuwa sababu mojawapo ya kuona umechelewa, hivyo hustahili kufanya jambo fulani katika umri fulani. Lakini kama unadhani kwamba kabla hujaondoka katika dunia hii, unatakiwa uwe umekamilisha ndoto yako au kusudi halisi la kuwapo duniani, basi msamiati wa kuchelewa unaweza kuwa sehemu ya maisha yako.

Wako watu wengi sana wanaofanya kazi ambazo kwa hakika wameshagundua hazitawafikisha wanakokutaka, lakini kinachowafanya waogope kubadili kazi hizo ni kuona kwamba wamekwishachelewa kubadili kazi hizo na hasa wengi ambao wameajiriwa katika maeneo mbalimbali.

Unapofika muda fulani kazini, unaona siwezi kubadili tena kazi na kwamba ngoja nistaafie tu huku, japo unajua ndoto zako hazijatimia na unafahamu wapi zingetimia lakini unaogopa kwenda, hujachelewa chukua hatua. Utajiri au mafanikio huwa yanakuja kama unavyokatika umeme bila tangazo la TANESCO!

Dhana ya kwamba umeshachelewa katika kupata mafanikio pia imewasababishia watu wengi matatizo makubwa. Wengine wamepoteza maisha kwa kufanya kazi haramu, kujidhalilisha, kuugua peresha, sukari na matatizo mengine ya kiafya na hasa pale wanapowaona rafiki, ndugu na jamaa wa karibu wakiwa na mafanikio makubwa, hata wengine ndoa zimevunjika kwa kukosa subira kwa kudhani mahala walipo si sahihi.

Ukweli ni kwamba tunapaswa kujifunza maisha kwa wengine lakini ni mwiko kuiga maisha hayo. Kila mtu ana siri ya mafanikio yake na wengi wanapoeleza juu ya mafanikio yao, huwa hawasemi ukweli na mara nyingi husema sehemu tu ya yale watu wanayoyaona juu yao.

Lakini ya sirini hayasemwi maana asili ya binadamu ni mbinafsi kwa hiyo si mara zote anapenda ufanikiwe kama yeye maana anataka tuheshimiane mjini.

Tunachopaswa kufahamu ni kwamba hakuna siku tutayawahi maisha, ndiyo maana hata wale wanaodhani wameyawahi hakuna siku wamepumzika kuyatafuta. Tutapumzika tu pale tutakapokuwa tumekata pumzi. Hata kama ungekuwa tajiri, profesa au kiongozi mwenye madaraka kiasi gani harakati zote hizo hazitakoma kwa kufanikiwa kimaisha bali kifo.

Ni kweli kwamba kila mtu anayahitaji maisha mazuri, lakini tusiyatafute kwa fujo kwa hofu kwamba tumekwishachelewa na hasa vijana wenzangu. Wakati mwingine sio kila nafasi inayotokea ni ya kutumia lazima tuwe na muda wa kutafakari kabla ya kuchukua hatua, vinginevyo tutasababisha matatizo makubwa sana katika jamii kwa kudhani kwamba kila ambaye hajafanikiwa hakutumia nafasi yake vizuri, lazima tukumbuke kila jambo lina wakati wake.

Hakuna binadamu aliyeko duniani kimakosa, suala la msingi ni kutafuta kusudi la kuwepo (purpose) ili ulitimize kabla ya kuondoka hajalishi una umri gani unaweza kufanya maajabu katika umri wowote na wakati wowote na historia yako ikaandikwa na pengine ukaacha msaada mkubwa sana kwa watakaobaki. Maisha ya jirani yako yasikuumize tafuta yako taratibu kila mmoja na fungu lake! Mbarikiwe nyote.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Watoto wa zamani viwanjani wa sasa kutwa 'play station'



Na Adam Fungamwango

**Cha kushangaza kwa sasa kuna utandawazi, lakini viwango vya wachezaji wa sasa ni vidogo ukilinganisha na vile vya wa zamani. Hii inatokana na kwamba baadhi ya wachezaji wetu wanaanza kucheza soka wakiwa na umri mkubwa. Na wanaanza kucheza soka baada ya kufeli sehemu mbalimbali za kutafuta riziki.**

KUNA wakati huwa wanawasikiliza wadau wa michezo wakitoa maoni yao juu ya kuzorota kwa michezo nchini kama vile soka, riadha na ngumi jinsi wanavyozunguka sana.

Wanaeleza vitu ambavyo ni sababu ya nne au ya tano. Lakini wengi hawaelezi sababu kuu ya kwa nini kwa sasa Tanzania imeshindwa kupata wanasoka bora au wanariadha bora.

Wakae wakijua kuwa huwezi kupata wanamichezo bora kama hawajazalishwa kutoka chini kabisa. Huwezi kupata mchezaji bora siku zote kama hakuna mipango thabiti.

Unaweza kupata mmoja au wawili baada ya miaka kumi. Huwa wanatokea kwa bahati tu. Ndiyo maana hadi leo kuna Mbwana Samatta tu. Amekuwa kama mtoto pekee kwa baba na mama. Ni kama mboni ya macho yetu. Anafuatiwa na Simon Msuva.

Hawa tunaweza kusema tu kuwa wametokea kwa bahati mbaya. Na wala hawakutengenezwa kwenye mfumo rasmi tangu walipokuwa wadogo.

Ukimsikiliza baba wa Samatta, mzee Ali Samatta, utajua kuwa mzee huyo ndiye alikomaa mwenyewe ili mtoto wake awe hivyo alivyo. Mzee huyo ukimsikiliza utajua kuwa alimlea mtoto wake ile wazazi wa zamani wanaita 'Kijerumani'.

Anaonekana kabisa kuwa ni mzee aliyekuwa na misimamo mikali kiasi cha kumlea mtoto wake kwa kutomdekeza.

Kwa sasa taifa la Tanzania halina wachezaji bora, wenye uwezo na vipaji vya hali ya juu kama zamani, kwani kabisa ni malezi ya wazazi. Wazazi wengi wa sasa wamekuwa wakiwadekeza mno watoto wao. Wanaogopa watoto wao wakicheza soka watavunjika miguu.

Hawataki watoto wao wapate shuruba ambazo wao walizipata wakati wakiwa watoto. Hapo ndipo tunapoanza kufeli.

Cha pili ni kutokuwa na viwanja vya michezo ambavyo kuna kipindi vilikuwa vinabinafsishwa au kuuzwa kwa kampuni, au matajiri ambao walikuwa wanabadilisha matumizi.

Sehemu ambazo zilikuwa viwanja vya kucheza watoto wa sasa vimegeuka nyumba za kulala wageni au gereji. Zamani nchi ilikuwa na wachezaji wengi mahiri kwa sababu wazazi walikuwa hawawazuii watoto wao kwenda kucheza au kuwafungia magetini.

Mfano wakati wa likizo, watoto watakutana na kufanya kikundi cha watu kuanzia kumi na kuendelea. Wataanza kutembea huku na huko wakitafuta viwanja pamoja na watoto wenzao na kucheza nao.

Vikundi vya watoto vinaweza kuwa hata sita. Watacheza hawa, wakifungwa wanatoka, wanaingia wengine kiasi cha kujikuta wanacheza kutwa nzima, kuanzia asubuhi hadi karibu na jioni, ndipo watakaporudi makwao.

Hali hii inakwenda mwezi mzima, hadi shule zitakapofunguliwa, watoto wanaanza kwenda mashuleni ambako huko watacheza tu michezo mbalimbali.

Kwa sehemu ambazo zilikuwa viwanja kwenye shule mbalimbali hasa za msingi, kumejengwa tena shule zingine. Watoto hawana pa kuchezea. Zamani kulikuwa na sehemu za kupumzikia, maarufu kama 'garden' ambapo mbali na michezo ya watoto kama mabembea, lakini pia kulikuwa na viwanja vya soka. Kwa sasa hakuna.

Miaka ya 1970 hadi 1990, huwezi kutembea mitaa mitatu au minne hakuna uwanja wa soka.

Hii iliwafanya watoto wengi waonyeshe vipaji vya tangu wadogo na hata wanapokuwa wacheza soka, au wanariadha wanakuwa wenye viwango vya juu kiasi cha kuifanya nchi kupata sifa.

Lakini pia ilisaidia hata maumbile ya wachezaji kujengeka kimichezo kwa sababu walianza tangu wakiwa wadogo.

Cha kushangaza kwa sasa kuna utandawazi, lakini viwango vya wachezaji wa sasa ni vidogo ukilinganisha na vile vya wa zamani. Hii inatokana na kwamba baadhi ya wachezaji wetu wanaanza kucheza soka wakiwa na umri mkubwa. Na wanaanza kucheza soka baada ya kufeli sehemu mbalimbali za kutafuta riziki.

Kama mchezaji ameandaliwa tangu mdogo kuwa mcheza soka, tusingeweza kuona hadi leo baadhi ya wachezaji hata kutuliza mpira tu wanashindwa wakati hilo ni somo la msingi kabisa ambalo mchezaji anatakiwa kujifunza wakati anaanza soka akiwa mdogo.

Wazazi wa sasa wanapowafungia watoto wao magetini na kutowaruhusu hata kucheza, hawawasaidii bali wanatakiwa kuwaacha ili waonyeshe vipaji vyao.

Zamani ilikuwa ni kawaida wakati hata mvua inanyesha kuwaona makundi ya watoto wakijitosa na kufurahia kwa kuimba na kucheza 'mvua njoo katarina usije' na baada ya mvua kumalizika wanakwenda kubadilisha nguo zao bila matatizo na maisha yanaendelea.

Leo hii huwezi kuona hilo, ambapo wazazi wengi wa sasa wanadai kuwa wataumwa, huku wakitetea kuwa maisha ya zamani na ya sasa ni tofauti. Lakini hawa hawa wazazi ndiyo wanaolalamika kuwa soka letu au michezo nchini Tanzania kwa ujumla imeshuka.

Hawa hawa wazazi ndiyo walionunua maeneo ya wazi, lakini hawa hawa ndiyo ambao wanawakataza watoto wao kucheza michezo mbalimbali, badala yake kuwaacha tu ndani wacheze 'play station.'

Hapa ndipo tunapofeli. Na kama wazazi wakiendelea hivyo, basi hata timu zetu za Tanzania zitaendelea kusajili wachezaji wengi kutoka nje ya nchi kwa sababu wenzetu huko bado kuna viwanja vya michezo na hawadekezi watoto wao kwenye malezi, kama ambavyo wazazi wa zamani walivyokuwa hawawadekezi watoto wao.

# HADITHI

## HADITHI

NEEMA ni mwanamke aliyeamua kuolewa ili atulie. Lakini ndani ya ndoa kuna raha na karaka. Ni uvumilivu tu ndio unaotakiwa, wakati mwingine uamuzi mgumu. Neema anakutana na mitihani ya hali ya juu, ambayo anajuta hata kuzaliwa. Mumewe Benson naye anakuwa moja ya matatizo kwenye ndoa hiyo. Kumbe kabla ya kumuoa alikuwa na mwanamke mwingine ambaye alitelekezwa. Mwanamke huyo, Halima, anaamua kuiweka ndoa hiyo kwenye tafrani na kuifanya isiwe na amani. Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu-1

**Na Adam Fungamwangwo**
**(0716 350534)**

JOTO la Dar es Salaam liliwaka kama pasi. Kila mmoja alihitaji kitambaa cha kujifutia jasho. Wengine walionekana kupita barabarani wakiwa na miavuli. Haikuwa miamvuli ya mvua bali ni ya kujikinga na jua. Wako waliokuwa hawajali hilo. Hakuwa na vitambaa vya kujifutia jasho. Hao walipita barabarani huku wakivuja jasho kama vile kijito kinavyotiririsha maji.

Ilikuwa maeneo ya kituo cha Keko jijini Dar es Salaam, kituo cha mabasi ya kwenda Kariakoo, Makumbusho, Magomeni na sehemu zingine. Eneo hilo liliitwa Keko Bora. Ilikuwa kweli barabara kubwa ya kutoka Mbagala, Uwanja wa Taifa kwenda Ilala.

Ilikuwa saa tano asubuhi. Lakini jua lilipiga kiasi cha kuonekana kama ni saa saba au nane mchana.

Baadhi ya abiria walikuwa wamesimama wakisubiri mabasi au daladala ya kuelekea wanakokwenda. Baadhi walikuwa wanazungumza, wengine walikuwa peke yao.

Hakuna aliyelitulia shaka gari aina ya Toyota IST lililofika kituoni hapo na kupaki mbele kidogo ya kituo hicho.

Ilionekana kama dereva alishuka na kwenda kununua kitu kando ya kituo hicho. Wengine walidhani kuwa ni mtu tu ambaye aliomba lifti alikuwa anashuka na kufika sehemu ambayo anakwenda.

Mtu mmoja mrefu alishuka. Alikuwa amevaa miwani myeusi. Alikuwa na nywele nyingi na alionekana mtanashati kiasi cha kutomtoa mtu yoyote wasiwasi.

Alikwenda eneo ambalo alitaka kwenda. Alipofika hakuna aliyeona alivyotoa bastola kwa haraka sana. Akanyoosha mkono wake juu na kupiga risasi tatu juu. Sauti ya risasi hizo zilirindima kwenye kituo chote cha Keko na maeneo jirani.

Aliyeonekana amekaa au kulala, basi alikuwa ameishiwa nguvu. Kila mmoja alitimua mbio. Hakukuwa na msalie mtume. Harufu ya hatari tayari ilikuwa inanukia. Tayari shari ilishaanza kunuka.

Baadhi walidandia daladala ili kuepukana na kifo kwa sababa wengi wao hawakuona ni nani aliyefanya vile. Mlio la risasi peke yake ulitosha kuwakimbiza bila kutaka kufahamu ni nani na anataka nini.




**Yeyote aliyedhani kuwa alikuwa jambazi aliyekwenda hapo kupora watu pesa au kupora pesa kwenye vibanda vya mawakala wa simu, au maduka alikosea. Alichofanya ni kwenda kwa mwanamke mmoja ambaye alikuwa na miaka usiyozidi 25. Mwanamke huyo alikuwa amemshika mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja hivi.**

Wakati wengine wakidandia daladala kukimbia hatari, waliokuwa kwenye daladala nao waliteremka chini, baadhi kwa kupitia dirishani.

Walidhani labda majambazi wamevamia daladala kwa ajili ya kutaka kuwapora. Hiyo ilitokea na daladala zote zilizokuwa eneo hilo

ili mradi tu ilikuwa tafrani juu ya tafrani.

Ndicho alichokuwa akihitaji yule mtu mweupe mrefu.

Alikuwa amevaa koti la bluu, ndani akiwa na fulana nyeupe, suruali aina ya jeans na raba za rangi ya bluu.

Yeyote aliyedhani kuwa alikuwa jambazi aliyekwenda hapo kupora watu pesa au kupora pesa kwenye vibanda vya mawakala wa simu, au maduka alikosea.

Alichofanya ni kwenda kwa mwanamke mmoja ambaye alikuwa na miaka usiyozidi 25. Mwanamke huyo alikuwa amemshika mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja hivi.

Milio ya risasi ilikuwa imeshamchanganya mwanamke yule, hivyo ilikuwa rahisi mno kwa mtu yule kumpora mtoto huyo na taratibu kurejea kwenye gari alilokuwa ameshuka. Ilikuwa kama mwewe hivi aliyempora kuku kifaranga.

Mkono mmoja akiwa ameshikilia mtoto, mkono mwingine ukiwa umeshika bastola iliyokuwa tayari kukohoa kwa yeyote yule atakayeonekana kutaka kukwamisha mipango yake.

Mlango ukafungwa na gari aina ya IST lenye rangi ya bluu likaondoka eneo hilo kwa madaha na kuwaacha watu wakizidi kuweweseka.

Hakuna yoyote yule aliyenakili namba. Kila mtu alikuwa anatafuta nafasi ya kujiokoa nafsi yake kwenye mdomo wa mauti.

"Mama mwanangu." Ilikuwa sauti ya kwanza kusikika, dakika tano baada ya milio mitatu ya baslota.

"Mwanangu jamani, wamemchukua mwanangu." Sauti ya kilio cha mwanamke ilizidi kuchukua nafasi yake, huku kila mmoja bado akiwa amegubikwa na hofu.

Pembeni ya mwanamke huyo alisimama mwanamume mmoja aliyekuwa amevaa fulana ya kijani na suruali ya mazoezi.

"Baba Diana, nimenyang'anywa mtoto." Ni sauti iliyomshtua mwanamume huyo aliyekuwa bado amepigwa na butwaa asiamini kile kilichotokea.

"Unasemaje mama Diana?"

"Diana kachukuliwa mume wangu, mama yangu weee Diana wangu..." Mwanadada alizidi kuangua kilio.

Ndipo taratibu baadhi ya watu walipoanza kurejea kwenye eneo la tulio, baada ya kujidhihirisha kuwa hapakuwa na hatari tena.

Baba Diana aliona yote yaliyotokea. Ambacho hakukiona ni jinsi gari lilivyopaki tu. Lakini alimwona yule jamaa mrefu alivyomsogelea mkewe. Wakati akishangaa. Aliona jamaa yule akitoa bastola, ndipo akili yake ikampaa na woga kumwingia.

Woga ulimpofusha macho kiasi cha kushindwa kuona nini kimetendeka.

Sauti za risasi tatu pia zilizidi kumchanganya na kumtisha. Mara ya mwisho alichoona ni gari ya IST kuondoka, kabla ya mkwewe kupiga mayowe.

"Dada nini kimetokea." Mmoja wa watu waliokuwa kwenye umati uliojitokeza hapo baada ya jamaa kuondoka aliuliza.

"Mimi nilikuwa nimesimama hapa na mume wangu huyu, akaja mtu mmoja mrefu, akapiga risasi juu na kuninyang'anya mtoto, akaondoka naye." Alisema dada huyo ambaye sasa alikuwa amekaa chini kabisa baada ya kuonekana kukosa nguvu kutokana na woga, kulia na kufadhaika. "Huwezi kuwa unamfahamu mtu huyo?" Mwigine aliuliza.

"Hapana simfahamu, halafu pia alikuwa amevaa mawani." Alijibu kwa kwikwi.

"Basi hapa cha kufanya kwanza kabisa ni lazima kwanza mkapige ripoti polisi mengine yafuate baadaye." Mwingine alidakia.

"Wewe ndiye mume wa huyu dada?" Bado watu walizidi kuuliza maswali.

"Ndiyo, tulikuwa tumetoka nyumbani, mtoto alikuwa anaumwa na hivi tulikuwa tunampeleka hospitalini, hapa tulikuwa tunasubiri daladala kwenda Hospitali ya Amana, lakini ndiyo tumekutana na haya yaliyotukuta." Alisema aliyeonekana kuwa ni mume wa dada aliyeporwa mtoto. Hapo sasa kila mmoja alikuwa na tafsiri yake.

"Inaonekana labda jamaa kaja kumpora mtoto wake, labda huyo mumewe kabambikiwa tu, jamaa anazinguliwa mtoto wake, sasa kaamua kuja kumchukua kwa nguvu."

Hizo zilikuwa dhana baada ya tukio hilo la aina yake kutokea. Katika sakata hilo ni mtu mmoja tu aliyeliona tukio hilo kwa usahihi zaidi.

Alimwona dada huyo na mumewe walivyokuwa wamevuka barabara na na kwenda hadi kituoni. Aliliona vizuri gari lilivyokuwa limepaki na mtu yule walivyoshuka na kumfuata dada aliyekuwa na mtoto.

Hadi mtu yule alivyopanda kwenye gari alimwona vizuri zaidi. Na wala hakutetemeka sana na milio ya risasi kwa sababu eneo ambalo alikuwapo asingeweza kudhurika.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# MPENI BUKU GIGY MONEY AMNUSURU AMBER RUTTY

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Gigy Money, amewaomba wanamtandao wa Instagram, kuchangia Sh. 1000 kwa kila mmoja ili kumnusuru Amber Rutty na mumewe, kuendelea kutumikia kifungo.

Gigy Money ameongea hilo baada ya kwenda Live kupitia ukurasa wake wa mtandao huo ambapo amesema kuwa

"Nimem-miss Amber Rutty hivi ndiyo atolewi tena, miaka mitano jamani tuchangeni Instagram tucheke tukichanga bukubuku tunamtoa Amber Rutty atakuwa ameshajifunza jamani, tuchangeni tuwatoe wale" amewaambia mashabiki wake.



# BARNABA
## AMJIBU KIADABU BABA YAKE

MWANAMUZIKI staa wa muziki wa Bongo Fleva, Barnaba Classic, ameamua kujibu kufuatia video fupi inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii ikimuonyesha baba yake mzazi akilalamika kwamba hapati msaada kutoka kwake.

Akizungumzia suala hilo, Barnaba Classic, amekiri kuwa yule aliyeonekana katika video ni baba yake mzazi, lakini anachokiamini hana tatizo lolote na baba yake mzazi.

"Yule ni baba yangu mzazi kabisa wala sio jambo la kiki , waswahili wanasema mzazi hakosei, hasemwi na hakosolewi, ukiachana na hayo mnayoyasikia mimi sina tofauti wala matatizo na baba yangu, namshukuru Mungu kwa kila jambo ila sitaki kulizungumzia sana suala hili, nilikuwa sijui kinachoendelea" amesema Barnaba Classic

## Prince Harry, Meghan wazidi kujazwa noti

WANAFAMILIA wa ufalme wa Uingereza ambao wapo katika mchakato wa kujitoa, Prince Harry na mkewe Meghan Markle, wamelamba dili nono la katika mtandao wa Spotify.

Mkataba huo wenye thamani ya Paundi za Uingereza milioni 30 ambazo sawa bilioni 92, unaanza kufanya kazi baadaye mwezi huu.

Awali mwezi Septemba mwaka huu, iliripotiwa kwamba wamelamba mkataba mwingine mnono kutoka kutika mtandao wa Netflix.

Netflix imeingia mkataba kwa ajili ya kutengeneza maudhui mbalimbali ikiwemo makala, filamu, na Vipindi ukiwa na thamani ya Dola Milioni 100 ambazo sawa na takriban Sh. bilioni 231.



# RASHFORD KUSAINI MKATABA MPYA



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inapanga kumpa mkataba mpya na mnono, Marcus Rashford, kwa mujibu wa Daily Star.

Mkataba wa sasa wa Rashford na Man United unamalizika mwaka 2023 na hivyo wanaangalia uwezekana wa kumpa mpya.

'Mashetani Wekundu' hao wameripotiwa kwamba, wanataka kumpa mkataba mnono zaidi Rashford ili aendelea kubaki hapo kwenye viunga vya Manchester.

Rashford amekuwa na kiwango cha kuvutia pale kwenye dimba la Old Trafford tangu alipoanza kuichezea kwa mara ya kwanza United mwaka 2015.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, katika mkataba huo mpya anaweza kupewa mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki.

# BUSQUETS AINGIA ANGA ZA MESSI

**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa Hispania, Sergio Busquets, ameingia kwenye rekodi mpya za Barcelona, baada ya kucheza michezo zaidi ya 500, tangu alipopandishwa kwenye kikosi cha kwanza mwaka 2008.

Busquets mwenye umri wa miaka 32, ameingia kwenye rekodi hiyo, baada ya kufikisha idadi ya michezo 594, aliyocheza klabuni hapo, huku akimshusha beki na nahodha wa zamani wa Barca, Carles Puyol katika nafasi ya nne kwa wachezaji walioichezea Barcelona michezo mingi zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Kiungo huyo alifikisha idadi hiyo ya michezo alipokuwa sehemu ya kikosi cha Barcelona kilichopambana dhidi ya Real Sociedad waliposhinda 2-1 katikati ya wiki.

Miongoni mwa michezo 594 ya Busquets, imetokana na ushiriki wake kwenye michuano sita duniani.

Michezo 390 ya Ligi ya Hispania (La Liga), 117 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, 64 ya Kombe la Mfalme (Copa del Rey), 15 ya Super Cup, mitano ya Klabu Bingwa Dunia na mitatu ya Super Cup ya Ulaya.

Mchezaji huyo alicheza mchezo wake wa kwanza akiwa na miaka 20, Septemba 13 msimu wa 2008/09, chini ya kocha, Pep Guardiola dhidi ya Racing na Barcelona walifanikiwa kuchukua mataji matatu msimu huo.

Wanaoongoza kwenye orodha ya wachezaji waliocheza michezo mingi wakiwa na Barcelona ni Xavi Hernandez (767), Lionel Messi(747), Andreas Iniesta (674), Sergio Busquets (594) na Carles Puyol (593).





# Kinda Mcameroon aweka rekodi mpya Bundesliga

**DORTMUND, Ujerumani**

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Youssoufa Moukoko, ameweka rekodi ya kuwa mfungaji wa kwanza mwenye umri mdogo zaidi kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Moukoko aliweka rekodi hiyo wakati Borussia Dortmund ikichezea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Union Berlin, usiku wa kuamkia jana.

Moukoko ambaye ni mzaliwa wa Cameroon na mchezaji wa timu ya Taifa ya Vijana ya Ujerumani, alifunga bao hilo akiwa na umri wa miaka 16 na siku 28.

Aliivunja rekodi ya awali iliyowekwa na Florian Witz wa Bayer Leverkusen ya miaka 17 na siku 34.

Dortmund wako katika nafasi ya nne, pointi sita nyuma ya vinara Bayer Leverkusen ambao jana Jumamosi walikuwa wanacheza na mabingwa watetezi, Bayern Munich.

Berlin wako katika nafasi ya tano pointi moja nyuma ya Dortmund.

RB Leipzig ambao wako katika nafasi ya tatu, walitarajiwa kucheza jana dhidi ya Köln.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH: NAWEZA KWENDA MADRID AMA BARCELONA

Nafikiri hizo ni klabu kubwa, nani anajua nini kitatokea baadaye, lakini kwa sasa akili yangu...

**LIVERPOOL, ENGLAND**

NYOTA wa Liverpool, Mohamed Salah, amekataa kuondoa uwezekano wa kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid au Barcelona.

Salah amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi tangu alipojiunga na Liverpool akitokea AS Roma mwaka 2017, akiwaongoza 'Wekundu' hao kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu England.

Nyota huyo wa kimataifa wa Misri amekuwa akihusishwa na uwezekano wa kuondoka hapo Anfield na kutimkia kwa miamba ya Hispania, Madrid na Barca.

Alipoulizwa kama ameondoa uwezekano wa kwenda LaLiga, Salah aliiambia Diario AS: "Nafikiri Madrid na Barcelona ni klabu kubwa.

"Nani anajua nini kitatokea baadaye, lakini kwa sasa akili yangu ni kushinda tena taji la Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya nikiwa na Liverpool."

Alipoulizwa kwa muda gani ataendelea kucheza Liverpool, Salah alijibu: "Hilo ni swali gumu, lakini kwa sasa naweza kusema kila kitu kipo mikononi mwa klabu.

"Bila shaka nataka kuvunja rekodi hapa, na narudia, rekodi zote za klabu, lakini kila kitu kipo mikononi mwa klabu."

Salah amefunga mabao 11 kwenye Ligi Kuu kwa Liverpool msimu huu, baada ya kufunga wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Tottenham katikati ya wiki.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amefunga mabao 14 kwenye mashindano yote msimu huu.

Liverpool inaongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa pointi tatu (kabla ya mechi za jana) dhidi ya Tottenham baada ya mechi 13.

## KWA UFUPI

**RASHFORD KUONGEZWA MKATABA**
MSHAMBULIAJI wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 23, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2023, anajiandaa kusaini mkataba mpya na Manchester United. **(Mirror)**

**DYBALA, FEDERICO NA UNITED**
NYOTA wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27, na kiungo wa Italia, Federico Bernardeschi mwenye miaka 26, ni miongoni mwa wachezaji waliopewa ofa na Manchester United wakati Juventus ikiangalia njia ya kumsajili tena kiungo Paul Pogba, 27. **(ESPN)**

**ANCELOTTI AMTAKA KHEDIRA**
KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, ameonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo, Sami Khedira, mwenye umri wa miaka 33 kutoka Juventus. **(Mail)**

**BUSSOUMA KUTUA LIVERPOOL**
KIUNGO wa Brighton na Mali, Yves Bissouma, mwenye umri wa miaka 24, anafuatiliwa kwa karibu na Liverpool kuelekea usajili wa Januari ili kuziba pengo la kiungo Georginio Wijnaldum, 30, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto. **(ESPN)**

**INTER YAJITOSA KWA WIJNALDUM**
INTER Milan imeingia kwenye mbio za kuwania saini ya Georginio Wijnaldum mwenye miaka 30, ambaye anawaniwa na Barcelona. **(Tuttomercato)**

**LINGARD HUYO SHEFFIELD**
KLABU ya Sheffield United inawania kumsajili straika wa Manchester United na England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28 kwa mkopo Januari. **(Manchester Evening News)**

**OZIL KUBAKI ARSENAL**
KIUNGO Mesut Ozil anapanga kubakia Arsenal hadi mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu, licha ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, kuwaniwa na klabu kadhaa ikiwamo Fenerbahce. **(Eurosport)**

**KABAK HAITAKI LIVERPOOL**
OZAN Kabak anayewaniwa na Liverpool, anakaribia kuamua hatima yake, na mlinzi huyo wa Schalke mwenye umri wa miaka 20 raia wa Uturuki, anataka kwenda AC Milan. **(Express)**

**FERNANDES KUONDOKA SPURS**
KIUNGO wa Tottenham Hotspur na Ureno, Gedson Fernandes, mwenye umri wa miaka 21, ataondoka Spurs Januari. **(Jornal de Noticias, via Sport Witness)**

**CITY KUMUUZA ZINCHENKO**
KLABU ya Manchester City inajiandaa kusikiliza ofa kwa mlinzi wake wa kushoto, Oleksandr Zinchenko mwenye umri wa miaka 24. **(90 Min)**

**PALACE KUMUUZA TOMKINS**
KLABU ya Crystal Palace ipo tayari kumuuza kiungo wake, James Tomkins mwenye umri wa miaka 31, huku kocha mpya wa West Brom, Sam Allardyce akihusishwa kumuwania mchezaji wake huyo wa zamani. **(London Evening Standard)**

**LIVER KUMGOMEA ELLIOT**
LIVERPOOL haina mpango wa kumuuza winga, Harvey Elliot mwenye umri wa miaka 17, ambaye anacheza kwa mkopo pale Blackburn Rovers. **(Liverpool Echo)**



# MKWASA: AZAM INABAHATI KUEPUKA KIPIGO KWA RUVU

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI mashabiki wa Azam wakilia na sare ya mabao 2-2, iliyopatikana juzi Ijumaa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijiji Dar es Salaam, huku Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Vivier Bahati akiwaangushia lawama wachezaji wake, mwalimu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa amesema wapinzani wao walikuwa na bahati, kwani kikosi chake kingeongeza utulivu kingeondoka na ushindi si chini ya mabao 4-2.

Akizungumza na gazeti hili jijini juzi usiku katika Uwanja wa Azam, baada ya mechi hiyo kumalizika, Vivier alisema wachezaji wao wamekuwa wakifanya makosa binafsi na kuwapa nafasi wapinzani kusawazisha.

Alisema makosa waliyoyafanya katika mechi iliyopita dhidi ya Namungo na kutoka sare ya mabao 2-2, yamefanana na waliyofanya dhidi ya Ruvu Shooting juzi. "Tunapata mabao magumu sana, lakini tunaruhusu kufungwa mabao mepesi, hiyo haisababishwi na mbinu za kocha mpya, ni kutokana na unapowapa maelezo wanaenda kufanya tofauti," alisema Vivier.

Alisema ana imani Kocha Mkuu, George Lwandamina, ameona upungufu huo na ataufanyia kazi mapema ikiwamo kuongea na wachezaji, lakini pia suala la usajili kipindi cha dirisha dogo.

Azam imecheza mechi nne mfululizo na kuambulia sare, dhidi Biashara United na Gwambana FC ugenini kabla ya kuzikaribisha Namungo FC na Ruvu Shooting katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam na kutoka sare ya mabao 2-2.

Kwa upande wa Mkwasa, alisema wachezaji wake wangekuwa wanaachiana mipira kwa haraka, wangewafunga Azam mabao mengi. "Mechi ilikuwa ya kwetu kabisa, tungekuwa tunaachiana mipira kwa haraka tungeweza kupata mabao mengi, lakini hizi dakika za mwisho za kipindi cha pili tumekosa mabao mawili ya wazi ambayo yangeweza kutupatia ushindi kabisa," alisema Mkwasa.

Baada ya sare hiyo, mashabiki wa Azam walikitupia kikosi hicho lawama nyingi kwa kushindwa kuwapa raha wakati wakitoa sapoti zote kama mchezaji wa 12 uwanjani ikiwa ni pamoja na kununua jezi za timu hiyo.

## KAZI INAANZA...



Mshambuliaji wa Kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta, anayechezea Fenerbahce ya Uturuki, akiwa ameanza mazoezi mepesi, baada ya kuwa nje kwa muda sasa akiuguza majeraha. Hadi sasa Samatta amecheza mechi saba tu na kufunga mabao mawili tangu ajiunge na timu hiyo msimu huu. **PICHA: MTANDAO**

# Bondia Class aanza kuuwinda ubingwa WBF

**Na Mwandishi wetu**

BONDIA nyota nchini, Ibrahim 'Class' Mgender, ameanza rasmi mazoezi ya kumwinda mpinzani wake, Mmalawi Dennis Mwale, lengo likiwa ni kutwaa mkanda wa dunia wa uzito wa Light unaotambuliwa na Shirikisho la Ngumi za Kulipwa Duniani (WBF).

Mabondia hao watapanda jukwaani Januari 29, mwakani kwenye ukumbi wa kisasa wa Next Door Arena uliopo Masaki jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na mwandishi wetu mwishoni mwa wiki, Class alisema amemsoma mpinzani wake na kugundua kuwa ni bondia mkali, hivyo imemlazimu kuanza mazoezi mapema chini ya kocha wake, Habib "Master" Kinyogoli.

Alisema mazoezi hayo yanafanyika kwenye Gym ya Amana, Ilala na anatarajia kuweka kambi rasmi ili kujiweka sawa katika pambano hilo ambalo limedhaminiwa na Kampuni ya Azam Media Limited.

Class alisema kwa sasa umebaki mwezi mmoja tu ili pambano hilo lifanyike kutokana na Desemba kuwa una siku za nyingi mapumziko.

"Nimeamua kuanza mazoezi mapema ili kujiweka fiti, mpinzani wangu ni mzuri, ili kujiweka sawa na kulinda heshima ya nchi, nimeanza mazoezi ya stamina na baadaye yatafuata ya ufundi," alisema Class.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mtendaji wa Jackson Group Sport, Kelvin Twissa, alisema wameanza maandalizi ya pambano hilo ambalo litakuwa la pili kwa kampuni yao kuandaa. "Tumeanza maandalizi ya pambano hilo na tunauweka ukumbi katika mandhari ya kisasa zaidi na mashabiki watakuwa kama wapo MGM Grand Las Vegas, Marekani," alisema Twissa.

Alisema siku hiyo kutakuwa na mapambano mengine makali ya utangulizi ambapo bondia wa kike wa Tanzania Stumai Muki atazichapa na bondia wa Zimbabwe Revai Madondo katika uzito wa fly wa raundi sita.

Pia kutakuwa na pambano kali kati ya bondia kutoka Kenya, Rayton Okwiri ambaye ataonyeshana kazi na Jimmy Mabundji wa DR Congo katika uzito wa Middle wa raundi nane wakati bondia nyota wa Tanzania Shaaban Jongo atazipiga na Mmarekani Shawn Miller katika uzito wa Cruiserweight la raundi 10.

Twissa alisema pambano lingine litakuwa kati ya bondia Nasibu Ramadhan dhidi ya Nkosinathi Biyana wa Afrika Kusini katika uzito wa Feather la raundi 10.

# Kipigo 3-0 fedheha kwetu - Mbeya City

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mbeya City imesema imesikitishwa na kufedheheshwa na kipingo cha mabao 3-0 ilichokipata kutoka kwa Biashara United kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma mkoani Mara juzi, Ijumaa.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Shaha Mjanja amesema hayakuwa matokeo mazuri hasa ukizingatia kuwa walitoka kucheza dhidi ya Simba na kufungwa kwa tabu bao 1-0 Jumapili iliyopita, huku wakicheza kandanda safi na la kuvutia.

"Tumeyapokea matokeo kwa masikitiko makubwa, tumetoka kucheza mchezo wa maana na Simba, tumecheza vizuri, lakini leo tumekuja kufungwa mabao 3-0 kwenye mechi ambayo wachezaji wetu hawakucheza kama walivyocheza dhidi ya Simba. Ni jambo linalofedhehesha sana," alisema Mjanja.

Alisema hata kocha wao mkuu Mathias Lule, ambaye ilikuwa ni mechi yake ya pili kukiongoza kikosi hicho, ameonyesha kusikitishwa jinsi wachezaji walivyocheza, kwani hawakujituma na kucheza kama alivyotarajia.

"Kwenye mechi dhidi ya Simba wachezaji wetu walicheza kwa namna ya kushangaza sana, walicheza kwa kujituma na uwezo wa hali ya juu, lakini mechi hii mambo ndiyo hivyo tena kama ilivyotokea, itabidi tujitazame," alisema msemaji huyo.

## Yanga Princess yazidi kutesa Ligi Wanawake

**Na Saada Akida**

YANGA Princess wameendelea kuonyesha kuwa wana jambo lao msimu huu baada ya kuendeleza kipigo kwa timu pinzani za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara.

Kikosi hicho kinachonolewa na Kocha Mkuu, Edna Lema, akisaidiwa na Mohammed Hussein 'Mmachinga' kimekuwa kikifuata nyayo za kaka zao ambao wanaongoza Ligi Kuu Bara na kuzifanya timu hizo za mtaa wa Twiga na Jangwani zote kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo hadi sasa msimu huu.

Katika kuonyesha msimu huu wamedhamiria kutwaa ubingwa, juzi kikosi cha Yanga kikiwa ugenini kiliibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya ES Unyanyembe, mabao yakifungwa na Grace Yusuph (2), Fatuma Bushiri, Philomena Daniel na Emiliana Mdimu.

Kocha Mkuu wa Yanga, Edna, alisema ana imani ligi itakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu timu zote zimejipanga kuonyesha ushindani mkubwa.

"Malengo yetu ni kutwaa ubingwa msimu huu, hivyo tunaenda kupambana kuhakikisha tunapata pointi kila mechi," alisema Edna.

Yanga Princess ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 13, ikifuatiwa na JKT Queens yenye alama 12 huku Simba ikishika nafasi ya tatu kwa pointi zake 11.

# Michezo

Jumapili Desemba 20, 2020

Nipashe




**Salah: Naweza kwenda Madrid ama Barcelona**

HABARI UK 22

## Simba vs Majimaji, Yanga na Singida FA

**Na Somoe Ng'itu, KIGOMA**

MABINGWA watetezi wa Kombe la FA Tanzania Bara, wataanza kampeni ya kutetea ubingwa wa mashindano hayo msimu huu kwa kuwakaribisha Majimaji FC kutoka Songea katika mchezo wa raundi ya tatu utakaochezwa mwishoni mwa mwezi huu.

Bingwa wa mashindano hayo hupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo hufanyika kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Msimu uliopita Simba ilifanikiwa kutwaa taji hilo lakini kwa sababu ilitetea pia ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, nafasi yake ilichukuliwa na Namungo FC ya Lindi ambayo ilikubali kichapo cha mabao 2-1, katika mchezo wa fainali uliochezwa Agosti 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo iliyochezeshwa jana mjini hapa, Yanga itawakaribisha Singida United kutoka Singida wakati Magereza FC itawafuata Azam FC huku Namungo FC ikiwavaa Green Warriors ya jijini Dar es Salam.

Ruvu Shooting yenyewe itacheza dhidi ya Mlale FC ya Ruvuma, Coastal Union itawaalika Stand United huku Dodoma Jiji wakiwavaa Hollywood FC ya Songea, Geita Gold itasafiri kuwafuata Mtibwa Sugar wakati JKT Tanzania itachuana na Magic Pressure na KMC FC itacheza dhidi ya Lipuli FC.

Hatua hiyo itaendelea tena kwa Biashara United kuwaalika Pan African huku Gwambina FC ikikutana na Usalama FC ya Dodoma, Kagera Sugar itawavaa Pamba FC wakati Mwadui FC itawasubiri Boma FC ya Mbeya huku Mawenzi ikipambana na Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela na Polisi Tanzania itawakaribisha Ndanda FC.

Mbao FC wao watawakaribisha Njombe Mji, Cosmopolitan wataivaa Tunduru, Mbeya Kwanza watawaalika Mashujaa United, Alliance FC watawakabili African Lyon, Kengold itachuana na Chato Stars, Amboni Stars itacheza dhidi ya Sahare Stars huku Kurugenzi FC wakiwafuata Kitayosa na ndugu wote wa Tanga Kwamndolwa watachuana na African Sports.

**WATAKIONA...**



Wachezaji wa Simba, Kiungo mnyumbulifu, Clatous Chama na beki wa kati, Joash Onyango (kulia), wakiwa mazoezini Harare nchini Zimbabwe jana, kujiandaa na mechi ya raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji FC Platinum, itakayopigwa Jumatano ijayo kwenye Uwanja wa Taifa wa Zimbabwe. **PICHA: SIMBA**

# NTIBAZONKIZA ANOGA YANGA AKIIPA USHINDI

●●●Aizima Dodoma Jiji akitupia moja na kutengeneza lingine, Lamine Moro azidi kuweka rekodi...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU akitokea benchi kipindi cha pili, kiungo mshambuliaji mpya wa Yanga, Mrundi Saidi Ntibazonkiza, ameonyesha hakuja Yanga kutalii baada ya kuifungia bao moja na kutengeneza lingine wakati ikiibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Dodoma Jiji jana.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, hadi Ntibazonkiza anaingia timu hizo zilikuwa zimekwenda mapumziko matokeo yakiwa bao 1-1.

Mabeki wawili wa timu hiyo, Lamine Moro na Bakari Mwanyeto, kila mmoja alifunga bao moja, huku Ntibazonkiza hiyo ikiwa mechi yake ya kwanza kuichezea timu hiyo kwenye Ligi Kuu na kufungua akaunti yake ya mabao.

Lakini pia lilikuwa ni bao lake la pili, baada ya lile alilofunga kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Singida United.

Ikitumia uwanja huo kama wake wa nyumbani, badala ya Benjamin Mkapa ama Uhuru jijini Dar es Salaam, Yanga ilishtukizwa bao la dakika ya nne, baada ya krosi ndefu iliyopigwa kulia mwa uwanja kumkuta kipa Metacha Mnata ambaye aliudaka na kuundunda bila kuangalia, ambapo karibu yake kulikuwa na straika mzoefu nchini aliyewahi kuzichezea klabu ya Ruvu Shooting na Azam FC, Seif Abdallah Karihe, ambaye aliuwahi na kuupiga kichwa, ukajaa wavuni.

Bao hilo la ghafla liliwaamsha Yanga usingizini kwa kuanza kulishambulia lango la Dodoma Jiji kama nyuki, lakini wachezaji wengi wa timu hiyo walikuwa wamerudi nyuma kujihami zaidi baada ya kutangulia kufunga.

Yanga ilisawazisha dakika ya 27, bao likifungwa na kapteni wa timu hiyo, Lamine ambaye anafikisha mabao manne msimu huu, akiwa ndiye beki anayeongoza kwa kufunga kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu.

Aliupata mpira ndani ya eneo la hatari kutokana na mkwaju wa faulo iliyopigwa na Deus Kaseke akiwa hajakabwa vizuri na mabeki wa Dodoma Jiji, akageuka na kupiga shuti hafifu lililojaa wavuni.

Ntibazonkiza ambaye aliingia mwanzoni mwa kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Michael Sarpong, aliunyanyua umati wa mashabiki wa Yanga dakika ya 69 alipofunga bao la pili kwa mkwaju maridadi wa faulo iliyotokana na yeye mwenyewe kuangushwa nje kidogo ya eneo la hatari. Ni bao ambalo lilionekana kuwavuruga wachezaji wa Dodoma Jiji na kuanza kucheza bila malengo.

Kwa upande wa Yanga, iliongeza mashambulizi kwenye lango la wapinzani wao na kujipatia bao la tatu dakika ya 75 lililowekwa wavuni na Bakiri Mwamnyeto akiutendea haki mpira wa faulo uliopigwa na Ntibazonkiza ambao ulimkuta mfungaji aliyepiga shuti lililojaribu kuokolewa na kipa Kalambo, lakini ulimshinda nguvu na kujaa wavuni.

Dodoma Jiji ilikaribia kufunga mabao yao kama si kukosa umakini kwenye safu yao ya ushambuliaji dakika ya 55 na 64 kupitia kwa Dickson Ambundo ambaye alikuwa akiisumbua mno ngome ya Yanga.

Dakika ya 55 akiwa ndani ya eneo la hatari aliachia shuti kali lililookolewa na kipa Metacha, lakini kwenye dakika ya 64, mlinda mlango huyo alifanya kosa la kupiga mbele mpira dhaifu uliomfikia Hamisi Mcha ambaye alimsogezea Ambundo na kupiga shuti kali lililowababatiza mabeki wa Yanga na kurudi uwanjani.

Kwa matokeo hayo, Yanga bado imeendelea kuongoza msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikifikisha pointi 40 kwa mechi 16 ambazo imecheza, huku pia ikiendelea na rekodi yake ya kutopoteza mechi yoyote ile kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042